¹⁹ Kwa noire suku ya Jumapiri‡ ire lulemba, wanafunzi wajumulana. Warifungira miryango ti kamana wawopa wakulungwa wa Mayahudi. Kwa mpunde noure, Insa akingira akimira kati-kati yawo, akiwambira: "Salama iwe namwe!"²⁰ Bandi yakwamba javire, kawolotera mmakono na mumbavu. Ikisa wanafunzi ware wákiwa radi pakulu sana kwa kummona Mwenye. ²¹ Insa akiwambira tena: "Salama iwe namwe! Namuna mmoja noyo kamba Baba vyaanipereke, omi novyo nukuperekani umwe."²² Nakwisa kwamba javire, akiwawesezera akiwambira: "Mpokerereni Roho Takatifu. ²³ Mukiwaswamii wanu dambi zawo, newo waswamiiwa. Mukitowa kuwaswamii, newo awaswamiiwa."

Insa na Tamimu

²⁴ Tamimu (zina rake rengine wakwitiwa "Masa") mwanafunzi mmoja nkati ya kumi na wawiri ware, iye áwerepo paájire Insa. ²⁵ Kwa javyo, wanafunzi wengine ware ndi wakimwambira: "Ofwe timmona Mwenye!" Fala iye akiwambira: "Kamba siwonire vilaso vya misumari mmakono mwake, na kamba sinkumbure javi na cala cangu mwákigomezeriwa, na kamba simpamire mumbavu na makono angu, sishubutu kukubali."

²⁶ Airini bandi ya suku nane, wanafunzi wakijumulana tena nnyumba, na Tamimu ire ákiwapo munkonjo nomo. Miryango wáfungiriwa ti-ti-ti, fala Insa kengira, akimira kati-kati yawo, akamba: "Salama iwe namwe!"

²⁷ Ikisa akimwambira Tamimu: "Njo naco kuno cala cako-co, uwone canja cangu. Nipame mumbavu-mu na nkono wako. Asa kudanzira-ko, kubali!"²⁸ Tamimu akinjibu: "Mwenye wangu, Nlungu wangu!"²⁹ Insa

* **20:9** Kufafanula ka Insa ndi kusoweriwe nZaburi 16:10 na nZaya 53:10-12. Ona novyo Inusu 1:17.

† **20:17** Mana ake ndi wanafunzi. ‡ **20:19** Kigeregu: "suku yakwanza ya sumana".

akimwambira: “Uwe ukubali kwa kuwa kuniwona? Heri ka ware sawaniwona fala wangari kukubali.”

³⁰ Kusema kweli, Insa akitendanga alama nyengine mbere ya wanafunzi sazandikiwe nkitabumu, ³¹ fala evi vyandikiwa ipate mukubali kuwa Insa ndi Almasihi, Mwana wa Mwenyezimungu. Na kwa kunkubali iye, mupata mainsha julu ya mamulaka a zina rake.

21

Insa awalawirira wanafunzi wake Galileya

¹ Bandi ya evi vinu-vi, Insa kawalawirira tena upya wanafunzi wake lufuko ra Tanda ra Tiberiya. Vikuna javi: ² Wekala pamoja Ansumani Peduru, Tamimu (wakwitiwa “Masa”), Nataniyeli wa Kanaa ya Galileya, wana wa Zebedeyu, pamoja na wanafunzi wengine wawiri. ³ Ansumani Peduru akiwambira wenziwe ware: “Nankuka kuvuwa.”

Ewo wakamba: “Ofwe tukufulata tikakwavye.” Wakilawa wakiripakira mungalawa wakuka. Wavuwa usiku nzima, awapatire kinu.

⁴ Pakucere subuu, Insa ákiwa nlufuko, fala wanafunzi ware awakimmanyira. ⁵ Insa akiwadairi: “Wanangu, amumpatire inswi anta mmoja?”

Ewo wakijibu: “Iii, atipatire kinu.” ⁶ Iye akiwambira: “Tayani nyavu-zo upande wa nkono nriro-wo, mupata.” Basi, wakitenda novire, awakidirire kuvuta nyavu zire, konta zikoreka inswi nyingi futi. ⁷ Kwa javyo, mwanafunzi ákipendiwa pakulu na Insa ire akimwambira Peduru: “Ire Mwenye!” Ansumani Peduru paasikire kuwa ákiwa Mwenye, akivala nguwo zake sanasana (konta kávala nguwo za mwani), akirefya mbahari. ⁸ Wanafunzi wengine ware wakinfulata na ngalawa ire, wakipita wakivuta nyavu zire na inswi tapa-tapa, kamana awawere baidi na lufuko, wákiwa kiyasi ca pima miya.

⁹ Nakwisuka mungalawa mure, wasingana makala a moto na inswi pajulu. Íkiwapo novyo mikate. ¹⁰ Insa akiwambira: “Njoni nazo inswi aba zamuvuwire sambipa-zo.” ¹¹ Kwa javyo, Ansumani Peduru akingira mungalawa mure, akivutira nyavu zire kungulu. Zikoreka inswi ulu-ulu, kwisabu piya zikiwa inswi miya na amusini na natu. Ingawa zikoreka inswi nyingi, fala nyavu zire azipapuke. ¹² Insa akiwambira: “Njoni murye.” Aalawirire anta mwanafunzi mmojawapo waktuwakali kundairi: “Uwe nani?” Wakijiwa kuwa ndi Mwenye wawenye. ¹³ Insa akija akitwala nkate ure, akiwapa. Na inswi zire novyo akiwapa. ¹⁴ Bandi ya kufufuriwa ka wafwi, Insa akiwalawirira mara ka mara wanafunzi wake, eyi ndi íwere mara yatatu.

Insa na Peduru

¹⁵ Nakwisa kurya, Insa akindairi Ansumani Peduru: “Ansumani, mwana wa Yahaya, unipenda pakulu kuwapunda ewa piya-wa?”

Iye akijibu: “Aye, Mwenye, ukwijiwa kuwa omi uwe nukupenda.”

Insa akimwambira: “Warise makondoo wangu watoto-wa.” ¹⁶ Mara yapiri Insa akindairi: “Ansumani, mwana wa Yahaya, unipenda?”

Iye akijibu: “Aye, Mwenye, ukwijiwa kuwa omi uwe nukupenda.”

Insa akimwambira: “Wasunge makondoo wangu.” ¹⁷ Mara yatatu Insa akindairi: “Ansumani, mwana wa Yahaya, unipenda?”

Peduru akikimiwa konta kándairi mara ya natu, “Unipenda?” Basi akinjibu: “Mwenye, uwe ukwijiwa piya vinu. Ukwijiwa kuwa omi uwe nukupenda.”

Insa akimwambira: “Warise makondoo wangu. ¹⁸ Nukwambira kweli: paukiwa nnemba, ukivala nguwo zako, ukuka kaukisaka konse. Fala pausaka kuluvala, ukolosa makono ako, munu mwengine akuvaza nguwo, akukisa kautowa kusaka.” ¹⁹ (Insa kasowera javire ipate amwambire Peduru namuna vyaaja kufwa kuno akinsifu Mwenyemizungu.) Bandi yakusowera javire, iye akimwambira: “Nifulate!”

Insa na mwanafunzi waakimpenda pakulu

²⁰ Peduru kazungunuka, kammona nyuma kure mwanafunzi mmoja akipendiwa pakulu na Insa. Eyu ndi ire mwanafunzi ârinamire upande wa mumbavu wa Insa pawekare piya wakirya, âdairire javi: “Mwenye, asaka kukuzungunuka ndi wepi?” ²¹ Peduru pammonire mwanafunzi ire, akindairi Insa: “Mwenye, sambu eyu mwananlume-yu, cisaka kunkuna kinani?” ²² Insa akijibu: “Nikisaka kuwa ainshi mpaka niludi, uwe cukuyeri kinani? Uwe nifulate tu basi!” ²³ Eya masowero-ya enera kati ya wanafunzi, ewo wereriwa kuwa mwanafunzi ire aafwa. Fala Insa aambire kuwa aafwa, ila kaamba: “Nikisaka iye ainshi mpaka niludi, uwe cukuyeri kinani?”

²⁴ Eyu ndi mwanafunzi alavya ushahidi wa vinu-vi, na ndi noyu andike evi vinu-vi. Tukwijiwa kuwa ushahidi wake-wo wakweli.

²⁵ Na viwapo vinu vingi vyengine tena vyaatendire Insa. Inawa vinu-vyo vyandikiwa kimoja-kimoja, niwona kuwa duniya isiwepo ando yakutula vitabu vikisaka kwandikiwa-vyo.

Vitendo vya Roho Takatifu

Mwanzo

Eci kitabu-ci cilunga hadisi ya wafulati wa Insa, mwanzo wa wakati waludire kuka mbinguni. Julu ya Roho Ntakatifu, wanafunzi wakidiri kwereza Habari Ngema mwanzo wa Yerusalemu mpaka Yudeya, Samariya na piya ulumwengu. Pakwanza, Peduru akiwerezanga Injili Mayahudi. Ikisa wanu sawari Mayahudi wakisakula kunfulata Insa, na Paulu akiwerezanga Injili ewo julu ya safari nyingi zawenye inti baidi-baidi.

Kitabu ca “Vitendo” cukolota namuna mawalii vyawokise mbere kazi ya Insa Almasihi. Cilunga na vitabu vyengine vya Injili. Kitabu ca “Vitendo” candikiwa na Luka, na kandika novyo hadisi kuhusu mainsha a Insa. Candikiwa kiyasi myaka 62 mpaka 64 bandi ya Almasihi.

Tamaa ya kuja Roho Takatifu

¹ Mwenye Teyofilu, kwa kitabu cangu cakwanza canandike kuhusu Insa piya vyaanzire kutenda na kufunda, ² mpaka suku yaakweziwe mbinguni bandi ya kuwamuru mawalii wake wawatondore, julu ya Roho Takatifu. ³ Bandi ya tabu zake, Insa akirotanga mbere yawo, julu ya kutenda vinu vingi vyawenye vyakuwakikisha kuwa iye kawa hai. Kawalawirira muda wa suku arubaini, na akisowera nawo kuhusu ufalume wa Mwenyelimungu. ⁴ Paajumane nawo, kawalaizira javi: “Musilawe Yerusalemu, murindire tamaa ya Baba yamunisikire omi. ⁵ Kwa kuwa kweli Yahaya koza* na maji, fala umwe suku karibu mukuja koziwa na Roho Takatifu†.”

⁶ Sambu, ewo pawajumulane, wanza kundairi, wakamba: “Mwenye, nowo wakati-wo ndi pausaka kuludisiriwa ufalume Iziraeli?” ⁷ Iye akiwajibu: “Visukuyerini kwijiwa suku wala wakati waaturire Baba nkati ya mamulaka ake mwaneyewe. ⁸ Fala paasaka kukwingirani Roho Takatifu, mupewa uwezo na mukuwa mashahidi wangu, mwanzo wa Yerusalemu na Yudeya piya pamoja na Samariya na mpaka kaisirize duniya.”

⁹ Pesire kwamba javire, akikweziwa wakinang'aniza javi, na wingu rikinfina. ¹⁰ Pawakinang'aniza julu rungu-rungu novire wakimmona iye akikweziwa, mpunde noure walawirira wanu wawiri na mavazi melupa vú, ¹¹ wakiwadairi: “Umwe, wanu waGalileya, mbana munang'aniza julu rungu-rungu? Noyu Insa wamumonire akikweziwa mbere yenu akuka binguni, iye aludi kamba vyamummwene akuka binguni novyo.”

¹² Ikisa wanafunzi ware wakilawa pamwango pare, wakiludira Yerusalemu. Mwango-wo ukitiwa Mizaituni, uwa karibu na Yerusalemu, kitambo ca kilometuru moja. ¹³ Pawafikire Yerusalemu kure, wakikwera mpaka julu pansana nyumba yawarindire: Peduru, Yahaya, Yakobu, Andere, Filipi, Tamimu, Bartolomeu, Matwaya, Yakobu mwana wa Alufeu, Ansumani Zeloti‡ pamoja na Yuda mwana wa Yakobu§. ¹⁴ Piya ware wákijumananga wakitenda duwa pamoja na wanawaka, Mariyamu mamaye Insa, na wanduze Insa.

* 1:5 Wakati-wo wakoza kwa munu kutiwira mmaji. † 1:5 “Koziwa” mana ake ndi kwijaziwa nfululu Roho Takatifu kati ya mainsha. ‡ 1:13 Wazeloti cikiwa kipinga ca siyasa ca Mayahudi wakisudiye kuwashinda waRoma. § 1:13 “Mwana wa Yakobu” au “nduye Yakobu”.

Munu mwengine atondoriwa awe walii

¹⁵ Nozire suku zire, Peduru akimira kati ya wenziwe ware, jumula ya wanu wákiwa kiyasi ca miya na shirini, ¹⁶ akisema: “Jamaa zangu, ajuzi atimiziwe Mandiko vyaâsowera Roho Takatifu mbere julu ya Daudi kuhusu Yuda, nouy awalongoze wanadamu wanfungue Insa.

¹⁷ Yuda ákiwa nkati ya kipinga cetu, ákipata fungu ra eyi kazi-yi.” ¹⁸ (Na maripo apatire bila shariya, nzuruku wake uziwa uweru. Noparepare akisomoka akigwirira pansí, mwiri wake ukilumuka kati-kati, utumbo ukisololokera panja. ¹⁹ Vikunire vire, wanu wa Yerusalemu piya wakipata kwijiwa, kwa javyo, kwa luga yawo uweru ure ukitiwa “Akeldama”, mana ake “uweru wa damu”.)

²⁰ Peduru akizidi kusowera, akamba javi: “Kamana kitabu ca Zaburi* caândikiwa javi:

‘Nyumba yake isamiwe, asiwepo wakwikala.’

Ikisa tena cikwamba:

‘Munu mwengine ekare kiti cake.’

²¹ Kwa javyo, tǔjuzi tintondore mwananlume mmojawapo áwere nafwe wakati piya watiinshire na Mwenye Insa, ²² tangu paanzire koza Yahaya mpaka suku yaatwariwe Insa binguni, ipate awe shahidi pamoja nofwe wa kufufuka kwake.”

²³ Basi, wakiwatondola wanu wawiri: Matiya, na Yusufu akitiwa Barisaba akijiwikana kwa zina ra Zushutu†. ²⁴ Ikisa wakilebela duwa, wakamba: “Mwenye, uwe ndi wijiwa myoyo ya piya-wa. Basi, kati ya ewa wawiri-wa, tolotere wauntondore mmojawapo, ²⁵ ipate tikore naye kazi za uwalii, zaasire Yuda akuka mahala pake paanjuzire iye mwananyewe.” ²⁶ Basi wakitenda kura, ikingwirira Matiya. Javyo iye akisanganyiwa na mawalii kumi na mmoja ware.

2

Kwisuka ka Roho Takatifu

¹ Paifikire suku ya sherehe ya Pentekoshiti, piya wakijumulana. ² Kwa mpunde noure, ikisikirikana shauti kulawa binguni, kamba vyaivuma mepo nyingi kanguvu. We! Mepo ijala nnyumba mwawekare mure fo! ³ Na vikilawirira vinu vyakulanda malulimi a moto akawanyika, akiwesukira kila mmoja. ⁴ Piya ikiwejala Roho Takatifu, wakanza kusowera luga nyengine, kwa uwezo wa Roho Takatifu.

Kushanga ka wanu

⁵ Yerusalemu wákiwapo Mayahudi, wakuwajibu mambo a Mwenyezimungu, wakilawirira kila inti za ulumwengu. ⁶ Paasikirikane namalove wa shauti za wanu, wanu wajire ware wakijumulana nopare. Wakifazaika kwa kuwa kila mmoja akisikira kwa luga yake yaapongoreriwe.

⁷ Ewo washanga na watajabu, wakamba: “Paa, namunani? Wanu-wa piya waGalileya, sinovyo? ⁸ Sambí, iwa mwaja? Ofwe kwa kila mmoja asikiraja kwa luga yake yaapongoreriwe? ⁹ Ofwe tiwa wanu wa inti za Pariti, Medi, Elamu, Mezopotamiya, Yudeya, Kapadokiya, Pontu, Aziya, ¹⁰ Furujiya, Panfliya, Miswiri, upande wa Libiya karibu ya kaya ya Kireni, pamoja na wayeni wakulawa Roma. ¹¹ Mayahudi na wengine wakubali dini ya kiyahudi, wengine walawa Kereta, na wengine walawa Arabiya. Piya-fwe

* **1:20** Ona Zaburi 69:25; 109:8. † **1:23** “Zushutu” mana ake “shariya”.

tisikira kwa kila moja luga yake, ewo wakisowera vinu vikulu vyaajabu vyaakunishe Mwenyezimungu. Mwaja?”¹² Piya washanga na watajabu, wakidairiyana watupu: “Noci kinu-ci, mana ake kinani?”¹³ Fala wengine wakiwakejeli, wakamba: “Ware warewa!”

Utuba wa Peduru suku ya Pentekoshiti

¹⁴ Peduru akilamuka pamoja na mawalii kumi na moja ware, na kwa shauti ulu akamba: “Umwe Mayahudi na piya muri kwikala Yerusalemu, vijiwikane kwenu. Tengani masikiro-yo musikire canisowera.”¹⁵ Ewa wanu-wa awarewire, kamba umwe vyamuri kudanizira kamana eyi novi ora, ingari namapema!¹⁶ Kwasa javyo, evi ndi vire visemiwe julu ya nabii Yoweli:

¹⁷ ‘Mwenyezimungu kasema javi*:

Vikuja kukuna suku za mwinsho,
Roho yangu niwatawanyira wanu piya nroho zawo.
Wanenu, waka na walume, wakuja kubushuru,
wanemba wakuja kuwa na ruhuya ya mawoni,
na wakulungwa wakuja kulota.

¹⁸ Kweli-kwelini, watwana wangu, waka na walume,
nozo suku-zo Roho yangu niwatawanyira,
newo wakuja kubushuru.

¹⁹ Nikolota mambo a matajabisa julu binguni,
na pansu muardhi nikolota alama: ya damu, ya moto,
na ya mawingu a rosi ra kwinukala pi!

²⁰ Juwa rikwinukala pi na mwezi ukuwa mweundu pyū kamba damu,
kábulu sainafika suku ulu yakutukuziwa Mwenye.

²¹ Na itakuwa kila mwenyé kutaja zina ra Mwenye Insa, avushiwa.’ ”

²² Peduru akizidi kusowera, akamba: “Umwe walZiraeli, sikirizani ewu usowezi-wu: Insa nNazareti ákiwa mwananlume akikishiwe na Mwenyezimungu mbere yenu, kwa maajuza, matajabisa, na alama zaakunishe Mwenyezimungu julu yake kati yenu umwe, kamba vyamwijiwe.”²³ Eyu munu-yu, kwa sababu ya mpango kamili wakusudiye Mwenyezimungu na wijiwifu wake tangu mida, kaperekiwa mmakono mwa wanu sawana shariya wangomezera pansalaba. Iye mumulaya.²⁴ Fala Mwenyezimungu kansisimusa na kanlavya malwazo a kifo, konta eco acikidiri kunfunga iye.

²⁵ Kamana Daudi† kâsema kuhusu iye:
‘Daima nimmona Mola mbere yangu.
Kawa upande wa nkono nriri wangu,
ndimana sitikinyika.

²⁶ Kwa javyo, moyo wangu uwa radi
lulimi rangu rifurahi,
visitoshe mwiri wangu untumaini,

²⁷ kamana awasa roho yangu kuka Kuzimu,
aumwasa Ntakatifu wako kuvunda nkaburi.

²⁸ Unolotera njira za mainsha.

Utakunijaza radi kwa kuwa pamoja nami.’

²⁹ Jamaa zangu, vyema nukwambireni bila kukufisani kuhusu wawa yetu nkulu Daudi. Kweli, iye kafwa, kazikiwa, na kaburi rake riwa pamoja nafwe mpaka rero-vi.³⁰ Iye ákiwa nabii. Iye ákijiwa kuwa Mwenyezimungu

* 2:17 Ona Yoweli 2:28-32. † 2:25 Ona Zaburi 16:8-11.

kânlapira[†] kuwa, nkati ya ujukulu wake, mmojawapo akuja kwikala kiti cake ca ufalume. ³¹ Ndimana Daudi kâsowera kuhusu kufufuka ka Almasihi, sakunamba kukuna. [§] Iye kaamba kuwa aasiwe Kuzimu wala mwiri wake auvundire.

³² Insa ambiwa-yu Mwenyezimungu kanfufula. Ofwe piya tiwa mashahidi kuwa kweli. ³³ Kwa kuwa iye kâkweziwa, kekaziwa upande wa nkono nriri wa Mwenyezimungu, na kâpokerera tamaa ya Roho Takatifu ka Baba, iye katimiminira evi vyamuri kuwona-vi na vyamuri kusikira-vi.

³⁴ Kamana Daudi aapandire binguni, fala iye kâsema* javi: ‘Mola kamwambira Mwenye wangu:

Ikala nkono nriri wangu,

³⁵ mpaka niwatende maaduwi wako wawe sini, kamba gogo rakwirika maułu ako.’

³⁶ Ndimana walziraeli piya wejiwe sana-sana kuwa noyu Insa wamûgomezere pansalaba-yu, Mwenyezimungu kantula kuwa Mwenye na kantula kuwa Almasihi.” ³⁷ Wanu ware pawasikire javire, vikiwalwaza mmyoyo mwawo, wakindairi Peduru pamoja na mawalii wengine ware: “Jamaa zangu, epa titende mwaja?”

³⁸ Peduru akiwajibu: “Tubiyani, na kila mmoja oziwe kwa zina ra Insa Almasihi, ipate dambi zenu ziswamiwe. Na umwe mupokerera tamaa ya Roho Takatifu. ³⁹ Kamana eyi tamaa-yi yenu umwe, pamoja na wanenu, na piya wari baidi naye[†], kwa piya wenye kwitiwa na Mola, Nlungu wetu.”

⁴⁰ Kwasa javyo, iye ákilavyanga ushahidi na usowezi mwingi wawenye na akiwarimbisa myoyo, akamba: “Muvushiwe nkati ya eci kizazi kibaya-ci.”

⁴¹ Basi, wakubalire usowezi wake, woziwa noparepare. Na kwa noire suku ire, isabu ya wenye kunfulata Insa yongezeka kiyasi ca wanu alufu natu.

Umoja wa wenye kwamini

⁴² Ewo watengemana kifulata kufunda ka mawalii ware, kuno wakiinshi na umoja wakupendana, wakitenda Jambo ra Kumbukumbu, na wakilebela duwa pamoja. ⁴³ Mawalii ware wákitenda mambo a matajabisa na alama nyingi, ndimana wanu piya uwengira wofi. ⁴⁴ Piya wamwaminire Insa wákiwa pamoja na vinu vyawo wakitumira ka upamoja. ⁴⁵ Wákiuzanya ankiba za mali awo na vinu vyawákiwa nawo, wakawanyirana kwa kila munu na aja yake. ⁴⁶ Suku daima wákitengemana kwa moyo mmoja paluwanja ra Nyumba Takatifu. Na nyumba anta nyumba wakitongerana Jambo ra Kumbukumbu na furaha, ka moyo radi. ⁴⁷ Wakintukuza Mwenyezimungu, na wakisifiwa na wanu piya. Basi, kila suku Mwenye akongeza isabu ya ware wakija kuvushiwa.

3

Kuponesiwa ka munu wakuremala

¹ Nakisa, wakati wa kutenda duwa, Peduru na Yahaya wakikwera nNyumba Takatifu. ² Na ákiwapo mwananlume mmoja wakuremala kipongorero. Ákisukuriwanga, ákituriwa panryango wa Nyumba Takatifu paki-tiwa “Nryango Mwema” akiwalebela zimola wanu wakingira nluwani ra Nyumba Takatifu mure. ³ Nakuwawona Peduru na Yahaya wari karibu

[†] 2:30 Ona 2 Samuweli 7:12-13; Zaburi 132:11. [§] 2:31 Ona Zaburi 16:10. * 2:34 Ona Zaburi 110:1. [†] 2:39 “Piya wari baidi naye” ndi Sawari-Mayahudi.

yakwingira nNyumba Takatifu mure, iye akiwalebela wammere zimola.
⁴ Peduru akinang'aniza rungu-rungu, pamoja na Yahaya, ikisa akamba: "Tinang'anize!"
⁵ Basi, iye akiwanang'aniza sana-sana, ákiwa na tamaa yakupokerera kinu kwawo.
⁶ Fala Peduru akamba: "Omi sina parata wala oru, fala caniri naco, nukupa. Kwa zina ra Insa nNazareti, lamuka enenda!"
⁷ Nakunkola nkono nrriro, akinlamusa. Kwa mpunde noure, mauu ake mmaluwata, akipata nguvu.
⁸ Upesi-upesi akimira, akanza kwenenda. Akingira nawo nNyumba Takatifu mure, akenenda, akidaruka, akintukuza Mwenyezimungu.

⁹ Basi wanu piya wammona akenenda akintukuza Mwenyezimungu,¹⁰ na wamanyira kuwa ndi noire ákikalanga paNryango Mwema wa Nyumba Takatifu, ákilebelanga zimola ire. Ndimana washanga na viwatikinisa vinku-nire iye vire, manshala!

Utuba wa Peduru nNyumba Takatifu

¹¹ Mwananlume aponesiwe ire, paankorire Peduru na Yahaya, wanu piya wakiwatuwirira ewo kapamoja mahala pakwitiwa "Lupenu ra Selemani", wakitajabu pakulu futi.
¹² Peduru nakuwona javire, akiwambira wanu ware: "Walziraeli wenzangu, mbena vyukushangishani kuwona evi? Mbana mutilavira maso ofwe kamba ndi timwenendese iye kwa uwezo wetu au ibada yetu?"
¹³ Nlungu wa Ibrahima na wa Izaki na wa Yankubu, Nlungu wa babu zetu, kantukuza ntumisi wake, Insa. Noyo-noyoni umwe wamumpereke aulaiwe na wamunkatare mbere ya Pilatu, ingawa kalangela kunfungula.
¹⁴ Fala umwe munkatala Ntakatifu, Mwenyé shariya, munlebela akufungurireni kisomi,
¹⁵ na mumulaya mwenyé kuwa nviriro wa uhai. Ila Mwenyezimungu kanfulula ka wafwi, na kwa eco, ofwe tiwa mashahidi.

¹⁶ Kweli, kwa kutumaini zina rake, eyu mwananlume wamummona na wamumwijiwa-yu, iwa kwa noro zina-ro ndi rimpatise nguvu. Kwamini kwake kuja julu ya Insa ndi cimponese nfululu mbere yenu.

¹⁷ Basi sambu, jamaa zangu, omi nukwijiwa kuwa mütenda kwa kutikina, kamba vyawátenda novyo mafalume wenu.
¹⁸ Fala iwa novyo-novyoni Mwenyezimungu vyaásowere tangu mida julu ya minabii piya, kuwa Almasihi wake ajuzi atabike, ndi vyaatimize namuna-yo.
¹⁹ Basi, tubiyani muludi, ipate madambi enu aswamiwe,
²⁰ na mupate wakati wakupumuzika kwa kuwa muwa pamoja na Mola, na iye akugabizini Almasihi Insa wamutuririwe tangu mida.
²¹ Iye ibidi ekare binguni mpaka wakati wakuludira vinu piya upya, kamba vyaasowere Mwenyezimungu tangu mida julu ya minabii watakatifu.
²² Kusema kweli, Musa kâsema javi: 'Mola Mwenyezimungu akuzushirani kati ya rikolo renu, nabii mmoja kamba omi.

Iye nsikirizeni piya caasaka kukwambirani conse.

²³ Na munu saansikiriza onse noyo nabii-yo, apoteziwa ndaraja ra umati.'

²⁴ Minabii wengine piya novyo, tangu Samuweli mpaka ware wajire nyuma yake, wereza viri kukuna ezi suku-zi.
²⁵ Umwe ndi ujukulu wa minabii na wa miyadi yakupatana yaturire Mwenyezimungu na wababu zenu, kâmwambira Ibrahima javi: 'Julu ya ujukulu wako, zijanliiwa piya kabila ziri mulumwengu-mu.'
²⁶ Ndimana Mwenyezimungu, paanfufure ntumisi wake Insa, kakuperekerani kwanza ipate akujanliyeni ajili ya kukutanusani, kila mmoja ase kukola dambi."

4

Peduru na Yahaya mbere ya Baraza ya Milandu

¹ Peduru na Yahaya, pawakisowera na wanu ware, wakiwalawirira walongozi wengine wa dini, nkulungwa wa minduna wa Nyumba Takatifu, pamoja na Masaduseu wengine. ² Ewa wakifazaika pakulu futi konta mawalii ware wakiwafunda wanu na wakiwereza kuwa kuwapo kufufuka ka kifo, julu ya Insa. ³ Ndimana wawakola wakiwafunga, wakiwataya nkal-aboshu mpaka subuu, konta juwa riswa. ⁴ Fala wengi wâsikire usowezi-wo wakubali. Isabu ya wanawalume wankubalire wakifika kiyasi ca alufu ntanu.

⁵ Iwa pakucere subuu, mafalume wawo, pamoja na wazee na wanlimu wa shariya wakijumana Yerusalemu. ⁶ Âkiwapo novyo Anasi, nkulu wa waku-lungwa wa dini, Kayafa, Yahaya, Alishandere, na piya wengine wawere jamaa za nkulu wa wakulungwa wa dini.* ⁷ Wakitumiza kuweta Peduru na Yahaya, wakiwemisa kati yawo, wakanza kuwadairi: “Mupata uwezoni au kwa zina ra nani vyamutendire-vi?”

⁸ Basi, Peduru wakumwijala Roho Takatifu, akiwajibu: “Umwe mafalume wenye inti pamoja na wazee, ⁹ ikiwa rero mwankutidairi kuhusu meema atendiwe kitewe-yu na musakula mwijiwe nani amponese, ¹⁰ bakini muk-ijiwa umwe pamoja na piya wanu wa Iziraeli, kuwa eyu mwananlume âri mbere yenu-yu kapona nfululu kwa zina ra Insa nNazareti, Almasihi. Noire wamûngomezere pansalaba ire, Mwenyezimungu akinfulula ka wafwi. ¹¹ Insa ndi ire asemwiwa nMandiko Matakatifu paamba javi: ‘Riwe ramukatatare umwe wajengi, mwinsho ndi riwe rikulu rifaire kujengera pamembe.’

¹² Kweli, hapana kuvuka julu ya mwengine tena, kamana aripo zina rengine sini ya binguni, rapewe mwanadamu, wakuwa ibidi ativushe ofwe.”

¹³ Sambi, wakulungwa ware, pawawawonire kurimba moyo Peduru na Yahaya, na pawejiwe kuwa wâkiwa wanu sawafyomire na sawasilimuke, ewo washanga na wawamanyira kuwa wakenendanga na Insa. ¹⁴ Fala pawammonire mwananlume aponesiwe ire ari pamoja nawo, awakidirire kufungula kanywa julu yawo. ¹⁵ Basi sambi, wakiwamuru walawe nnyumba ya Baraza ya Milandu ire, ewo wakibaki wakikaidiyana watupu, ¹⁶ wakamba: “Tiwatende mwaja nowa wanu-wa? Kamana wanu piya wa Yerusalemu wakwijiwa kuwa eya maajuzi-ya ewo ndi watendire, na ofwe atina vyakukaniza. ¹⁷ Epa, kwa kusakula habari-zi zisisikirikane ka wanu piya, tîjuzi tiwatishe wasisowere na munu asâka kuwa onse tena kuhusu noro zina-ro.” ¹⁸ Basi, wakitumiza kuweta tena, wakiwamuru kuwa wasisowere na wasifunde tena kwa zina ra Insa.

¹⁹ Falakini Peduru pamoja na Yahaya wakijibu, wakiwambira javi: “Lamulani umwe wanyewe. Cakweli ndi cepi mbere ya Mwenyezimungu? Tikusikirizeni umwe au Mwenyezimungu? ²⁰ Konta ofwe aitibidi kunya-mala, tîjuzi pakulu tisowere baina catiwonire na catisikire.” ²¹ Basi, waku-lungwa ware wakingira kuwopepesa tena, mwinsho wakiwafungula waki-wasa. Awawonire shariya ya kuvahukumu, konta piya wanu wakintukuza Mwenyezimungu kwa vinu vikunire vire. ²² Kamana, ire mwananlume

* **4:6** Anasi, nkewe Kayafa âkiwa na mamulaka pakulu koliko Kayafa. Kayafa wakati-wo âkiwa nkulu wa wakulungwa wa dini. Anasi âkiwa nkulu wa wakulungwa wa dini suku za nyuma.

ankunire maajuza akuponesiwa ire, ákiwa na umuri wa kupunda myaka arubaini.

Peduru na Yahaya na wenye kwamini wajumana kulebela duwa

²³ Peduru na Yahaya pawafunguriwe, wakiludira ka wenziwawo ware, wakiwereza piya vyawâmbiriwe na wakulungwa wa dini pamoja na wazee. ²⁴ Ewo nakusikira, wakilebela duwa pamoja ka Mwenyezimungu, wakamba: “Mola Nkulu, uwe ndi umbire bingu, ardhi, bahari, pamoja na viumbe piya viri nkati yake. ²⁵ Uwe kusowera kwa Roho Takatifu julu ya babu yetu Daudi†, ntumisi wako, ukamba:

‘Mbona Sawari-Mayahudi wankubishana na Mola? Mbona wanu wankupanga vinu savina kazi?’

²⁶ Mafalume wa mulumwengu wankuritengeza, wenye mamulaka wajumana,

wabishane na Mola pamoja na Waantawaze‡ iye.’

²⁷ Kweli, eyi kaya ulu-yi, Herodi na Pontiyu Pilatu wajumana na Sawari-Mayahudi pamoja na wanu wa Iziraeli, kubishana na Insa, ntumisi wako takatifu waantawaze. ²⁸ Ewo wajumana watende piya vyaupangire tangu mida kuwa vijuzi vikune. Kupanga javyo kwa sababu ya uwezo wako na kamba vyausakire. ²⁹ Basi sambu, Mola, ona kutisha kwawo, walavye wofi nfululu watumisi wako wereze habari zako. ³⁰ Tenda javyo kuno ukolosa nkono wako ipate uponese, na tenda alama na matajabisa kwa zina ra Insa, ntumisi wako takatifu.”

³¹ Pawesire kulebela duwa, mahala pawajumane pare patenda kitikansi. Piya akiwengira Roho Takatifu, wakanza kwereza habari za Mwenyezimungu bila wofi.

³² Kwa nkonjo wa ware waminire ware, piya wákiwa na mawazo mamoja na nafsi moja. Áwepo anta munu mmoja wakwamba kuwa evi vinu-vi vyangu omi, ila piya vinu vyawákiwa nawo, víkiwa vyawo. ³³ Kwa uwezo nkulu, mawalii wákilavya ushahidi wa kufufuka ka Mwenye Insa. Na rehema nyingi íkiwesukira wanu ware piya. ³⁴ Kamana noure nkonjo wa wenye kwamini ure, áwepo wakusakula kinu, kutowa kupata. Wákiwa na masamba au manyumba onse wakiuzanya, nzuruku ure wákijanga, ³⁵ wákiwagabizi mawalii mmakono mwawo, newo wákiwatongeranga wanu, kwa kila mmoja ákipata caasakula.

³⁶ Ákiwapo mwananlume akitiwa Yusufu, wa rikolo ra kinya Lawi, kâpongoriwa kisirwa ca Kiporo. Mawalii wántapira zina ra Barinaba, mana ake “mwenyé kutaya niya”. ³⁷ Kwa kuwa Yusufu ire ákiwa nawo ngwamba, iye kauzanya, ikisa nzuruku akija nawo, akiwagabizi mawalii mmakono mwawo.

5

Ulongo wa Ananiya na nkawake Safira

¹ Ákiwapo mwananlume mmoja akitiwa Ananiya. Iye na nkawake Safira wôzanya amana yawo, ² fala Ananiya, kasikizana na nkawake, nzuruku ure fungu rimoja akiriturira pambari, mwengine akiwagabizi mmakono mawalii.

† 4:25 Ona Zaburi 2:1-2. ‡ 4:26 “Waantawaze” ndi Almasihi.

³ Sambi, Peduru akindairi: “Ananiya, sababuni kumwasa Ibilisi kukidiri moyo wako kuntesa Roho Takatifu, kulavya nzuruku mwengine kuriturira pambari? ⁴ Kábula saunauzanya, kanzi-yo aiwere yako? Na bandi ya uzanya, nzuruku-wo auwere wako? Sambi, kinani cukuwazise mmoyo wanako kutenda javyo? Uwe aulongope ka wanadamu, kulongopa ka Mwenyezimungu!”

⁵ Ananiya, paasikire ewu usowezi-wu, akigwa rä, wakufwa wawenye. Na piya wasikire vikunire vire uwapata wofi pakulu futi. ⁶ Noparepare, wakija wanemba wakintwala, wakinkafini, wakinsukula wakuka wakinzika.

⁷ Bandi ya ora natu, akilawirira nkawake. Iye aákijiwa cinkunire nlumake. ⁸ Peduru akindairi: “Nganambire, ewu ndi nzuruku wamuzanye amana yenu?” Iye akijibu: “Aye, ndi nowu.” ⁹ Peduru akimwambira: “Sababuni uwe na nlumako kusikizana kuentavya Roho wa Mwenyezimungu? Basi, wanemba wanzikire nlumako ndi ware panryango pare. Nowe novyo wákusukula.” ¹⁰ Kwa mpunde noure, akingwira Peduru mmaulu rä, wakufwa wawenye. Wanemba ware pawengire wansingana wakufwa. Noparepare wakinsukula, wakuka wakinzika upande wa nlumake. ¹¹ Basi, wanu wa jamati*, na ware wasikire eyi habari-yi ware, piya uwapata wofi pakulu pawenye.

Alama na matajabisa a mawalii

¹² Alama na matajabisa mengi akikuna kati ya wanu, julu ya makono a mawalii. Newo piya wákiwa Lupenu ra Selemani na niya mmoja. ¹³ Wanu wengine awakitwakali kuringiza nowo nkonjo wawo-wo, fala wakiwasifu. ¹⁴ Kwa kila mara, nkonjo wa ware wákimwamini Mwenye ukizidi kongezeka, waka na walume wengi. ¹⁵ Kwa javyo, wanu wakija nawo walwere nvinanda na mmashila panja pare, ipate akipita Peduru, nanga kinviri cake ciwafinike walwere wamojawapo. ¹⁶ Wanu wengine tena wa kaya jirani za Yerusalemu wakija nawo walwere na wamizuka. Na piya ware wakiponesiwa.

Kulumbatiwa ka mawalii

¹⁷ Basi, nkulu wa wakulungwa wa dini, na piya wawawere nawo pamoja kati ya nkonjo wa Masaduseu, ukiwengira wiyana. ¹⁸ Ndimana wakiwafunga mawalii ware, wakiwataya nkalaboshu ya wafungwa piya. ¹⁹ Fala usiku, laika wa Mola kafungula miryango ya kalaboshu ire, akiwalavira panja, akiwambira: ²⁰ “Ukani kuNyumba Takatifu, mukawereze wanu habari piya kuhusu eya mainsha-ya.” ²¹ Ewo nakusikira javire, pakucere wakuka wakingira nNyumba Takatifu, wakanza kuwafunda wanu.

Sambi, nkulu wa wakulungwa wa dini akifika pamoja na ware waákiwa nawo. Ewo wakiwarifu wanu wa Baraza ya Milandu pamoja na wazee piya wa wana wa Iziraeli. Ikisa wakiwatuma minduna kukalaboshu kure ipate wakaje nawo mawalii ware. ²² Fala minduna ware, pawafikire kukalaboshu kure, awawasingane. Basi wakiludi, wakija, wakijibu: ²³ “Katukire kure tisingana miryango ya kalaboshu ifungiwe ti, na maamiri wekare panryango nopo. Fala patifungure, nkati atisingane anta munu mmoja.”

²⁴ Nkulungwa wa minduna wa Nyumba Takatifu na wakulungwa wa dini, pawasikire javire, wafazaika mama! Vikuna-vi ndi vyepi? ²⁵ Kwa mpunde

* 5:11 “Jamati” mana ake ndi nkonjo wa wenye kunfulata Insa.

noure, akifika munu mmoja akiwambira: “Onani! Wanawalume wamuwataire nkalaboshu mure ware, wemira nNyumba Takatifu, wankuwafunda wanu!”²⁶ Basi, nkulungwa wa minduna wa Nyumba Takatifu, akuka pamoja na minduna kuwatwala mawalii ware. Fala wawatwala bila kuwatendera nguvu, konta wakiwopa wanu kuwapanja na mawe.

²⁷ Pawawafikise kuBaraza ya Milandu, wakimisiwa mbere. Nkulu wa wakulungwa wa dini akiwadairi,²⁸ akamba: “Ofwe atukukatazeni kufunda kuhusu eri zina-ri, fala kweli-kwelini umwe mwankwijaza kila upande wa Yerusalemu kufunda kwenu, na musaka mutipatise lawama na damu ya noyu munu-yu!”²⁹ Peduru na mawalii wenziwe wakijibu: “Tíjuzi tinsikirize Mwenyezimungu koliko wanadamu.³⁰ Nlungu wa babu zetu kanfulula Insa wamámulaye mukungomezera pansalaba.³¹ Fala noyu, Mwenyezimungu kanlamusa upande wake wa nkono nrirō awe Nlongozi na Nvushi, ipate iye Mwenyezimungu waZiraeli awatubise na awaswamii dambi zawo.³² Ofwe tiwa mashahidi wa evi vinu-vi, na shahidi mwengine ndi Roho Takatifu. Iye ndi Roho Mwenyezimungu wawapa piya wenye kunsikiriza iye.”

³³ Wanu ware, pawasikire javire, wakimiwa pakulu futi, wakisaka wawolaye.³⁴ Falakini munkonjo wa Baraza ya Milandu mure, mwanlimu mmoja wa Taureti, Nfarizeu wakwitiwa Gamaliyeli, wakwinshimiwa na wanu piya, akamuru kuwa wanawalume ware walaviriwe panja wakati aba. Ikisa, akiwambira,³⁵ akamba: “Wenzangu walziraeli, more-moreni na ewa wanu-wa. Wazani sana-sana vyamuka kuwatenda-vyo.³⁶ Suku za nyuma, kálawirira mwananlume mmoja wakwitiwa Tehuda, akiritula kuwa munu bora. Iye káwapata wanu kiyasi ca miya nne. Fala mwinsho káulaiwa, na wanu wakifulata ware wakitawanyikana piya, nkonjo ure ukifujika.³⁷ Airini, suku zakwandikiwa marikolo, akija akilawirira Yuda, nGalileya. Iye novyo kákidiri kuwapata wanu wengi wawenye wakunfulata, fala neye novyo kólaiwa, na wakifulata piya wátawanyikana.³⁸ Basi, nukulebelani javi: ritanuseni na ewa wanu-wa, waseni woke kwa salama, konta ikiwa ewu mpango-wu ulawa ka munu, ufujika.³⁹ Falakini ikiwa ulawa ka Mwenyezimungu, umwe amukidiri kufuja, musije kuwoniwa kamba mubishana na Mwenyezimungu.”

Na ewo wakikubali vyaambire Gamaliyeli vire.⁴⁰ Sambu wakiweta mawalii, wakiwacapisa, wakiwakataza kuwa wasisowere tena zina ra Insa rire, na wakiwafungula.⁴¹ Kwa javyo, mawalii ware nnyumba ya Baraza ya Milandu mure walawa na moyo radi, konta Mwenyezimungu kawatula ubora wakejeliwe kwa sababu ya zina ra Insa.

⁴² Na daima-zi, nNyumba Takatifu na mwawákipita mmamanyumba, awakasa kufunda na kwereza kuwa Insa Almasihi.

6

Watondoriwa wanu saba wakuwavya mawalii

¹ Kwa nozire suku zire, pawazidire kongezeka wanafunzi wa Insa, íkiwapo dugudugu nkati ya Mayahudi wakuwera kigeregu na ware wakuwera kiebraniya. Ware wakuwera kigeregu wakiduguda kuwa manankweli wawo awanang'aniziwa sana pacitongiwa cakurya kila suku.² Ndimana mawalii kumi na wawiri wawajumanisa piya wanafunzi wa Insa, wakiwambira: “Sivyo vyema ofwe kwasa kufunda usemi wa Mwenyezimungu, kupita tikihudumu mmameza.³ Kwa javyo, kati ya wanduzetu-wa, watondoreni wanu saba wakuwa nawo ushahidi wakuwejala Roho Takatifu na

fahamu ipate tiwagabizi eyi kazi-yi. ⁴ Ila ofwe tishugulikire kulebela duwa na kufunda usemi wa Mwenyezimungu.”

⁵ Piya ware uwajibu usowezi ure. Wakintondola Shitefanu, wakolota kwamini pakulu na wakumwijala Roho Takatifu. Wakiwatondola tena Filipi, Porokoro, Nikanori, Timoni, Parmena, pamoja na Nikolayu wa Antiyokiya, akubalire dini ya kiyahudi. ⁶ Wanu ware wakolotiwa mbere ya mawalii, wakilebeleliwa duwa, na wakituriwa makono.

⁷ Basi sambu usemi wa Mwenyezimungu ukenera. Isabu ya wanafunzi Yerusalemu ikongezeka pakulu, na walongozi wa dini wengi wakisikiriza ka kwamini.

Kufungiwa ka Shitefanu

⁸ Shitefanu, kwa kumwijala rehema na uwezo, ákitendanga matajabisa makulu-makulu na alama mbere ya wanu. ⁹ Fala wakizuka wanu wamojawapo wa sinagoga ikitiwa “Ya wenye uhuru”. Wákiwa Mayahudi wa Kireni na Aleshandriya, na wengine wa Kilikiya na Aziya. Ewo wakanza kukaidiyana na Shitefanu. ¹⁰ Falakini ewo awakikidiri kunshinda wijiwifu tele-tele pamoja na Roho vikinsoweresa.

¹¹ Ikisa wawaripa wanu wengine wambe javi: “Tinsikira akikufuru ka Musa pamoja na Mwenyezimungu.” ¹² Wakiwashongezera wanu ware, wazee, na wanlimu wa shariya. Nakunfika karibu Shitefanu, wakinkola, wakinlongoza kuBaraza ya Milandu ya Mayahudi. ¹³ Noparepare, wakiwemisa mashahidi walongo wakisema: “Eyu mwananlume-yu aasa kukufurira mahala takatifu-pa pamoja na Taureti. ¹⁴ Kona tinsikira akisema kuwa Insa nNazareti-yo adangula mahala-pa na apindula tabiya zaatasire Musa.” ¹⁵ Na piya wanu wekare paBaraza ya Milandu ire, nakunang'aniza rungu-rungu, wammona uso wake ure kuwa kamba wa laika.

7

Kurikotola ka Shitefanu pamilandu

¹ Sambu, nkulu wa wakulungwa wa dini kandairi Shitefanu: “Uwe, kweli-kwelini ndi novyo?” ² Iye akijibu: “Jamaa zangu, wanduzangu pamoja na wawawa, sikirizani! Mwenyezimungu ntukufu kámwisukira wawa yetu Iburahima paákiwa Mezopotamiya, saanasamira kwikala Harani, ³ kámwambira javi: ‘Lawa inti yako, wase jamaa zako, uke inti yanisaka kukolotera yonse.’ ⁴ Ikisa, Iburahima akilawa inti ya waKaldayo, akuka akiinshi Harani. Nokurekure, bandi ya kufwa wawaye, Mwenyezimungu kansamisira Iburahima eyi inti yamuri kwikala umwe sambu-yi. ⁵ Mwenyezimungu ampere Iburahima kuriti, anta mahala pakutula mulu. Novyo-sivyo, iye kámpa tamaa ya kumpa inti-yi iye iwe yake-yakeni pamoja na ujukulu wake, ingawa áwere nawo mwana. ⁶ Mwenyezimungu akamba kuwa ujukulu wake wakuja kuwa wamalamboni wakwikala inti ya wanu wengine, wawe watwana, watabishiwe kwa muda wa myaka miya nne. ⁷ Tena Mwenyezimungu akamba: ‘Inti yawasaka kutendiwa utwana-yo, niwahukumumu. Ikisa, bandi ya evyo, wasama, wakuja kunitukuza omi epa mahala-pa.’ ⁸ Mwinsho akimpa miyadi ya kupatana julu ya itani. Kwa javyo, paamongore Izaki, akintaya itani suku yanane yawenye. Izaki akimpongola Yankubu, na Yankubu akiwapongola wanawe kumi na wawiri, wababu zetu wakulu.

⁹ Wababu zetu wakulu ware wantendera fitina nduyawo Yusufu, wamuzanya akuka inti ya Miswiri. Fala Mwenyezimungu ákiwa pamoja neye. ¹⁰ Iye akinlavya tafauti zake piya, akimpa fadili na wijiwifu mbere ya

Firyauna, nfalume wa Miswiri. Ndimana Firyauna akintawaza kuwa waziri wake Miswiri, na akingabizi nyumba yake ya kifalume.

¹¹ Ikisa ikija njala inti ya Miswiri na Kanaa piya, ikiwataya wanu mashaka makulu futi. Anta babu zetu awakipata cakurya. ¹² Fala Yakobu, paasikire kuwa Miswiri iwapo tirigu, kawatuma wanawe, wababu zetu, safari yakwanza. ¹³ Pawokire safari yapiri, Yusufu karijiwisa mbere ya wanyenyeze, na Firyauna akipata kuwejiwa jamaa zake Yusufu. ¹⁴ Yusufu akitumiza kumwita Yakobu wawaye na jamaa zake piya, isabu ya wanu sabini na watanu. ¹⁵ Basi Yakobu akiteremukira Miswiri, nokurekure akifwa pamoja na wababu zetu. ¹⁶ Airini, maiti awo aperékiwa Sikemi, kawazikiwe kaburi râuzire Iburahima kwa isabu ya parata na wakinya Emori Sikemi kure.

¹⁷ Wakati paufikire karibu, Mwenyezimungu katimiza tamaa yaâmpere Iburahima, kabila yetu Miswiri ikizidi kongezeka pakulu. ¹⁸ Sambu Miswiri kure katawala nfalume mwengine sakimwiwiza Yusufu. ¹⁹ Eyu kawatenyiza jamaa zetu, kawatabisha babu zetu julu ya kuwalazimisha wawase panja wasimana watoto wasiinshi.

²⁰ Kwa nowo wakati-wo ndi waapongoriwe Musa. Iye ákiwa mwema sana. Kareriwa myezi mitatu nnyumba ya wawaze, ²¹ na paasiwe toto ire, mwana wa Firyauna akinlokota, akinrera kamba mwanawe. ²² Musa kafundiwa wijiwifu piya wa Miswiri, na kawa mwenyé nguvu wa masemo na vitendo.

²³ Musa, paafikire hirimu ya myaka arubaini, akiwaza kuka kuwawona jamaa zake, waIzraeli. ²⁴ Paammonire muIzraeli mmoja akitabishiwa, iye akimwingirira, akiriripira kwa ire akitabishiwa ire, akinduru mMiswiri ire. ²⁵ Musa akiwaza kuwa wanduze waIzraeli wakwereriwa kuwa Mwenyezimungu awanusuru julu yake iye, fala awereriwe. ²⁶ Subuu yake akiwalawirira walizraeli wamojawapo wakumana. Akiyerera kuwapatanisa, akiwambira: 'He! Umwe muwa munu na nduye, mbena musausana watupu?' ²⁷ Fala munu akintabisha mwenziwe ire, akintanuka Musa, akiwambira: 'Uwe, akutawaze kuwa nkulungwa wetu waakutilamula nani?' ²⁸ Usaka unulaye novyo kamba vyaumulaye ijana mMiswiri ire?' ²⁹ Nakusikira javire, Musa akitira, akuka inti ya Midiyani kamba mmalamboni. Nokurekure akiwapongola wana wawiri.

³⁰ Ipita myaka arubaini, ari nlanga ra mwango wa Sinayi, kamwisukira laika na malulimi a moto, akikorera pafukutu. ³¹ Musa akishanga kwa ruhuya imwisukire ire, nakusengereza karibu awone sana, ikinjira shauti ya Mola, ikamba: ³² 'Omi ndi Nlungu wa kinya babuzo: Nlungu wa Iburahima, wa Izaki, na wa Yankubu.' Musa akanza kutetema, anta kunang'aniza aakishubutu. ³³ Mola akiwambira: 'Vula viratu vya mmaulu mwako-vyo, konta mahala pauri-po patakatifu. ³⁴ Niwonanga mashaka makulu awatabishiwa wanu wangu wari Miswiri, nisikiranga kiriro cawo. Ndimana nisuka niwafungure. Sikiriza sana-sana! Nankukutuma uludire Miswiri.'

³⁵ Noyo Musa wawânkatare-yo, ewo pawandairire javi: 'Nani akutawaze kuwa nkulungwa na mwenyé kulamula?', noyo noyoni, Mwenyezimungu kampereka kuwa nkulungwa na nvushi, julu ya laika âmwisukire pafukutu ire. ³⁶ Na noyo noyoni ndi awalavire wanu Miswiri, pesire kutenda matajabisa na alama inti ya Miswiri, Bahari Nyeundu, na nlanga, muda wa myaka arubaini. ³⁷ Noyo noyoni ndi Musa awambire walizraeli javi: 'Mwenyezimungu anzusha nkati ya wanu wake nabii wenu kamba vyanizushire omi.' ³⁸ Noyu ndi ire ákiwa pamoja nawo walizraeli wajumane

nlanga. Iye ndi awere shikarakanzi kati ya laika na kinya babu zetu kumwango wa Sinayi kure. Iye ndi apokerere usemi hai, akitipa ofwe.

³⁹ Fala wababu zetu awasakire kunsikiriza Musa, wankatala. Mmyoyo yawo, wakisaka kuludira Miswiri, ⁴⁰ wakimwambira Aruna*: ‘Titendere maswanamu wakutitongoza. Kamana Musa atilavire Miswiri-yo, atijiwa cinkunire.’ ⁴¹ Newo wakintenda swanamu, nfano wa ng’ombe ntoto. Ikisa, wakintendera kafara swanamu ire, na wakinsherehereka pakulu kinu cawantendire na makono awo. ⁴² Basi, Mwenyezimungu akiwatanuka, akiwasa wakambudu vyumbiwe binguni kamba vyavyândikiwe nkitabu ca minabii†, cisema javi:

‘Onani, walziraeli! Nlanga, muda wa myaka arubaini, munilavira omi kafara yenu na swadaka? ⁴³ He! Kwasa kutenda javyo, musukula ema ya Moleki‡, na nondwa ya swanamu Rafani, mifano yamutendire wanyewe mupate kwambudu. Sikweli?

Ndimana nukutuwisirani baidi kupunda Babiloniya.’

⁴⁴ Wababu zetu wákiwa nawo nlanga Ema ya Ushahidi, ijengiwa kamba Mwenyezimungu vyamwamurire Musa kujenga, kwa kifulata nfano waawonire. ⁴⁵ Wababu zetu wapokerera noire Ema ire, na wasukula pawalawire na Yoshwa kuriti intú-yi. Mwenyezimungu yaawatuwisire mataifa mengine mbere ya wababu zetu. Na Ema ire ikibaki nokure mpaka wakati wa Daudi. ⁴⁶ Iye karehemiwa na Mwenyezimungu, kanlebelana nafasi ya kuwatafitira walziraeli mamburo awo§. ⁴⁷ Falakini, ajire akijenga nyumba-yo ndi Selemani. ⁴⁸ Ka ukweli, Mwenye Nkulu ekala nyumba zaku-jenga wanadamu. Kamba vyêreze nabii mmoja*, akamba javi: ⁴⁹ ‘Binguni ndi kiti cangu, ardhi ndi yanirika maułu angu.

Ndi nyumbani yamusaka kunijengela? (amba ndi Mola).

Au mahalani panisaka kupumula?

⁵⁰ Sumi na nkono wangu mwaneyewe nitendire piya vinu-vi?’ ”

⁵¹ Shitefanu mwinsho akamba javi: “Umwe muwa wabishi, amukeketiwe myoyo yenu na murimba masikiro†. Daima munkatala Roho Takatifu, kamba vyawákinkatalanga wababu zenu. ⁵² Nabiini salumbatiwe na babu zenu? Ewo wawolaya mitume wákerezanga mida habari ya kwisuka ka Mwenyé shariya‡. Sambi, na umwe ndi novyo: munzungunuka, mumulaya iye. ⁵³ Nomwe-nomweni ndi mupokerere shariya ilawire ijire na malaika. Novyo-sivyo, umwe amutumire noyo shariya-yo.”

Vyaafwire Shitefanu

⁵⁴ Wakulungwa ware, pawasikire usowezi-wu, ukiwasoma mmyoyo mwawo, wakintafunira meno. ⁵⁵ Fala iye kamwijala Roho Takatifu, kanang’aniza binguni, kawona nuru ya utukufu wa Mwenyezimungu, na kammona Insa emire upande wa nkono nriri wa Mwenyezimungu. ⁵⁶ Neye akisema: “Onani! Nankuwona binguni wanzu, na Binadamu wa Binguni kemira upande wa nkono nriri wa Mwenyezimungu!”

⁵⁷ Fala nakukuwa pakulu, wakiziwa masikiro, wakimwirukira piya kwa niya mmoja. ⁵⁸ Wakintuwisira panja ya kaya ulu ire, kuno wakinpanja na

* **7:40** Aruna ákiwa nduye Musa. † **7:42** Ona Amosi 5:25-27. ‡ **7:43** Moleki ákiwa nlungu saári wakweli wa waKanaa. § **7:46** Kigeregu: “nyumba ya Yakobu”. * **7:48** Ona Izaya 66:1-2. † **7:51** Kigeregu: “Amutaiwe itani myoyo yenu na masikiro enu”, mana ake awasaka kusikiriza habari za Mwenyezimungu. ‡ **7:52** “Mwenyé shariya” mana ake Insa Almasihi.

mawe. Mashahidi wakinvula nguwo zake zaâvarire wakingabizi mmakono nmemba wakwitiwa Saulu.

⁵⁹ Ewo wakizidi kumwefya mawe, kuno Shitefanu akilebela duwa, akamba: “Mwenye Insa, pokerera roho yangu.” ⁶⁰ Ikisa akikokora, akifula uto, akamba: “Mola, usiwahukumu kwa eyi dambi-yi!” Pesire kusema javire, akifwa.

8

¹ Na Saulu kakubali kuulaiwa ka Shitefanu.

Saulu akwanza kuwalumbata wenye kwamini

Noire suku ire, jamati* Yerusalemu akanza kuwapata mashaka a kulumbatiwa pakulu. Piya wakitawanyikana inti za Yudeya na Samariya, ila mawalii awatirire Yerusalemu kure. ² Wanu mamuminu wanzika Shitefanu na wanririra pakulu futi. ³ Fala Saulu akifuja jamati ire, akingira nyumba anta nyumba, akiwasukuma waka na walume, akiwatayisa nkalaboshu.

Filipi akwereza Habari Ngema Samariya

⁴ Sambi, watawanyikane ware wapita wakereza Habari Ngema. ⁵ Filipi neye akiteremukira kaya moja ya Samariya, nokurekure akiwereza wanu kuhusu Almasihi. ⁶ Wanu wengi wakinsikiriza sana-sana Filipi vyaakisowera, wakinsikiriza kwa niya mmoja kuno wakiwona alama zaakitenda. ⁷ Kamana wanu wengi wakupatiwa na mashetwani, wakisomoka kuno wakituwisiwa mashetwani ware. Na vitewe pamoja na wakütumbela wengi wikiponesiwa. ⁸ Kwa javyo, nkaya mure ikiwapo radi pakulu futi.

⁹ Nokure, akiinshi mwananlume mmoja wakwitiwa Ansumani, mida âkitenda vitendo vya usawi, âkiwatajabisanga waSamariya. Iye akiritula ubora. ¹⁰ Piya wenye kaya ire kwanza ntoto mpaka nkulu wakinsikiriza, wakamba: “Eyu munu-yu kanawo uwezo wa Mwenyezimungu, kanawo uwezo Nkulu.” ¹¹ Ewo wakinsikiriza konta suku nyingi zawenye âkiwatajabisa na vitendo vya usawi. ¹² Fala pawankubalire Filipi vyaakereza kuhusu ufalume wa Mwenyezimungu na zina ra Insa Almasihi, wakanza koziwa, waka kamba walume. ¹³ Anta na Ansumani novyo iye mwanenye kakubali. Bandi ya koziwa, âkenendanga na Filipi. Iye, kwa kuwona alama na matajabisa makulu âkitendanga are, akitajabu.

¹⁴ Mawalii Yerusalemu, pawasikire kuwa waSamariya wakubali usemi wa Mwenyezimungu, wakiwapereka noko Peduru na Yahaya. ¹⁵ Pawafikire, wawalebelela duwa ipate wampokerere Roho Takatifu. ¹⁶ Konta noure wakati ure, âkiwa saanamwisukira munu anta mmoja. Ila ewo woziva kwa zina ra Mwenye Insa tu basi. ¹⁷ Basi, wakiwatula makono, newo wakimpokerere Roho Takatifu.

¹⁸ Ansumani, paawonire kuwa wankupewa Roho Takatifu julu ya kuturiwa makono na mawalii ware, neye akiwamera nzuruku, akamba: ¹⁹ “Nnomi novyo nipeni noyo mamulaka-yo, ipate wanintula makono onse, ampokerere Roho Takatifu.” ²⁰ Fala Peduru akimwambira: “Upoteya uwe pamoja na nzuruku wako-wo mwanenye! Kuwaza kuwa ruhuya ya Mwenyezimungu ipatikana kwa nzuruku?” ²¹ Uwe auna fungu wala upande kati ya eyi kazi-yi kamana moyo wako auri sana mbere ya Mwenyezimungu! ²² Basi, tubiya mabaya ako-yo, unlebele Mola, dalili akuswamii caulangele mmoyo mwako-co. ²³ Kamana niwona kuwa kwanawo nyongo ya wiyana

* 8:1 “Jamati” mana ake kundi ra wanu wakunfulata Insa Almasihi.

pakulu, na kuwa nkati ya kifungo ca ubaya.”²⁴ Ansumani akiwajibu, akamba: “Umwe-po nilebeleleni ka Mola ipate cisinikune kimojawapo vyamusowere-vyo.”

²⁵ Peduru na Yahaya, pawesire kulavya ushahidi na kwereza usemi wa Mola, wakiludira Yerusalemu. Pawakiludi, wakereza Habari Ngema makaya mengi a waSamariya.

²⁶ Ikisa, laika wa Mola akisowera na Filipi, akamba: “Lawa uke upande wa suheli, utware njira ya kuteremukira Yerusalemu ukukirira Gaza.” Noyo njira-yo yalanga. ²⁷ Basi Filipi akilawa akuka. Paakuka akisimanana naye mwananlume cande wa Etiyopiya, ákiwa ntumisi nkulu wa Kandasí†, Rainya wa Etiyopiya. Noyo mwananlume-yo ndi agabizwe piya kazi za mizuruku. Iye kôka Yerusalemu kuntukuza Mwenyezimungu. ²⁸ Paásimanane nawo-po ákiludira kwawo. Kekala munkukuta mwake, akifyoma kitabu ca nabii Izaya. ²⁹ Roho Takatifu kamwambira Filipi: “Sengereza karibu ya nkukuta ure pare, ukasikire nowe.” ³⁰ Filipi akituwa akisengereza pankukuta pare, akinsikira nEtiyopiya ire akifyoma kitabu ca nabii Izaya. Filipi akindairi: “Mwaja? Camufyoma-ci, mwankwereriwa?” ³¹ Amiri ire akinjibu: “Neriwaja saneleweshiwe?” Kwa javire, iye akimwambira Filipi, akamba: “Kwera munkukuta-mu, tikare onse.”

³² Usowezi takatifu‡ wawenye waákifyoma ndiwu, ukwamba javi: “Iye ákiwa kamba kondoo wakuka kusinjiwa, kamba mwana wa kondoo vyanyamala ndu, ka mwenye kunsinja mabururu ake, novyo-novyoni neye aambure kanywa yake.

³³ Kwa kurinyenyekeya kwake, wantuwa shariya. Hapana asaka kusowera kuhusu kizazi cake kônta uhai wake ulaviwa mulumwengu-mu.”

³⁴ Amiri ire akindairi Filipi: “Nukulebela, evi vyaamba nabii-vi kankuramba mwanyewe au munu mwengine mmojawapo?” ³⁵ Basi Filipi akanza kusowera, na mwanzo wa noya Mandiko Takatifu-ya, akimwereza habari ya Insa.

³⁶ Pawakuka munjira, wakisingana maji. Amiri ire akamba: “Are pare maji! Cikataza omi koziwa kinani?” ³⁷ § ³⁸ Basi, amiri ire akimisisa nkukuta ure, wakisuka wo-wawiri, wakingira mmaji, Filipi ire akimoza noparepare. ³⁹ Pawalawire mmaji mure, Roho wa Mola akinlainisa Filipi, na amiri ire awere wakumona tena. Basi, akitwala njira akuka vyake ka moyo radi! ⁴⁰ Filipi akiwoniwa Azoto, akipita akereza Habari Ngema kaya ulu-ulu zire piya mpaka akifika Kaisariya.

9

Insa amwita Saulu anfulate

¹ Saulu akizidi kutisha na mawazo a kuwolaya wanafunzi wa Mwenye Insa. Akimukira nkulu wa wakulungwa wa dini, ² kunlebelwa waraka ya kuka Damashiku akolote mmasinagoga, ipate akiwasingana walume au waka wenye kifulata Njira ya Insa, awafunge, oke nawo Yerusalemu.

† **8:27** “Kandasí” mana ake “Rainya”. ‡ **8:32** Ona Izaya 53:7-8. § **8:37** Mandiko mengine a mida eyi aya-yi aipo. [Filipi akinjibu: “Ukamini ka moyo wako piya, acipo cikataza.” Na iye akinjibu: “Nukwamini kuwa Insa Almasihi Mwana wa Mwenyezimungu.”]

³ Fala iye paakuka vikinkuna ari karibu ya Damashiku, kwa gafula ikinzunguriza nuru ya kulawa binguni. ⁴ Noparepare akigwa, akisikira shauti ikimwambira: “Saulu, Saulu, mbana unilumbata?” ⁵ Iye akidairi: “Uwe nani, Mwenye?”

Shauti ire ikinjibu: “Omi Insa waunlumbatanga-yo. ⁶ Fala lamuka, uke ire kaya ire, eko ukwambiriwa caukujuzi kutenda.”

⁷ Wanawalume walongozane naye Saulu ware, wakimira wakinyamala, wakisikira shauti fala awakimmona munu wawenye. Mashala! ⁸ Saulu akilamuka pansi pare, na ingawa maso ake kafungula, fala aakiwona kinu. Ndimana, ewo wakinkola nkono, wakimukisa Damashiku. ⁹ Iye kekala suku natu saawona. Nozo suku-zo, aataire pakanywa cakurya wala maji.

¹⁰ Damashiku kure akiwapo mwanafunzi mmoja wakwitiwa Ananiya, imwisukira ruhuya ya Mwenye Insa, shauti ikimwita: “Ananiya!” Iye akijibu: “Labeka, Mwenye.” ¹¹ Mwenye Insa akimwambira: “Ritengeze, uke barabara yakwitiwa Koloka. Ukafike nyumba ya Yuda, ukandairishe mwananlume wa Tarusu wakwitiwa Saulu. Ka ukweli, iye kankulebela duwa. ¹² Imwisukira ruhuya, neye kammona mwananlume wakwitiwa Ananiya akingira akintula makono, akinlebelela aludire kuwona.”

¹³ Ananiya akijibu: “Mwenye, niwasikiranga wanu wengi wawenye wakisowera kuhusu noyo mwananlume-yo na ubaya mwingi iye awatendanga wanu wako watakatifu Yerusalemu-ko. ¹⁴ Na epa iye kanawo mamulaka a wakulungwa wa dini a kuwafunga piya wenye kwambudu zina rako.”

¹⁵ Fala Mwenye kamwambira: “Uka, konta noyo mwananlume-yo nintondola nintumire awereze zina rangu Sawari-Mayahudi, mafalume, pamoja na walZiraeli. ¹⁶ Omi mwananyewe nimolotera Saulu mashaka akija kunkuna kwa ajili yangu.”

¹⁷ Basi Ananiya akuka, akingira nyumba ire, akintula makono, akamba: “Nduyangu Saulu, Mwenye kanituma kwako, Insa mwananyewe akulawirire munjira-yo, ipate uludire kuwona na akwijare Roho Takatifu.” ¹⁸ Kwa mpunde noure, vigwa vinu mmaso mwa Saulu vyakulanda mamba a inswi. Kweli, iye akiludira kuwona. Basi, akilamuka akuka akoziwa. ¹⁹ Pesire kurya, akipata nguvu.

Saulu Damashiku

Saulu akikala Damashiku nokure pamoja na wanafunzi wa Insa kwa munda wa suku aba. ²⁰ Kwa wakati noure, akuka mmasinagoga a Mayahudi, akanza kwereza kuhusu Insa, kuwa iye ndi Mwana wa Mwenyezimungu.

²¹ Piya wakinsikira, wakitajabu, wakamba: “Sinoyu mwananlume akiwalumbata wambudu zina ra Insa Yerusalemu kure-yu? Scinjisire epa noco, awafunge, awapereke ka walongozi wa dini?” ²² Fala Saulu kila mara akizidi kwijaziwa uwezo. Iye akiwatikinisa Mayahudi wakikala Damashiku kwa kuwejiwisa kuwa Insa ndi Almasihi.

²³ Zipita suku nyingi zawenye, ²⁴ Mayahudi wakisikizana kumulaya, fala iye kawejwirira mipango yawo. Ikisa tena, Mayahudi wakisonderanga mmiryango ya kaya, usiku na nsana, ipate wammone Saulu wamulaye. ²⁵ Ndimana, wanafunzi wake wakintwala usiku, wakimpenyeza pakitololo ca kipama, wakinteremusa.*

* **1:5** Ona 2 Samuweli 7:14; Zaburi 2:7. † **1:5** Ona 2 Samuweli 7:14. ‡ **1:6** Ntanzi akiwa nriti wa vinu piya vya wawaye. § **1:6** Ona Kumbukumbu 32:43. * **1:7** Ona Zaburi 104:4.

watumisi wake wawe kamba malulimi a moto.”

⁸ Fala kuhusu Mwanawe, akwamba javi†:

“Uwe Mwenyezimungu, útawala daima milele.

Úwatawala wanu muufalume wako kwa shariya.

⁹ Kwankupenda ukamilifu na wankukukima ubaya.

Kwa javyo, omi Mwenyezimungu, Nlungu wako, nukumiminirani mafuta a radi pakulu koliko wenziwo piya.”

¹⁰ Mwenyezimungu kamwambira Mwanawe tena‡:

“Mwenye, tangu mwanzo, uwe ndi uturire aluserusu ya duniya, na kwa makono ako kumba bingu piya.

¹¹ Evyo piya-vyo vilainika, fala uwe kuwapo daima.

Avija kufāi kinu, kamba nguwo zakupapuka.

¹² Kamba zubāu ya mīda, ndi vyauja kukunja, kamba munu vyaaluriza nguwo, uwapindula.

Fala uwe ndi nowe wa daima, kuinshi kwako akuna mwinsho.”

¹³ Mwenyezimungu laikani wamwambire suku moja javi§:

“Ikala mahala bora-pa upande wangu wa nkono nriro-wu, mpaka maaduwi wako niwature kumaulu kwako”?

Malaika-wo wa kinani? ¹⁴ Piya-wo siroho zintumika Mwenyezimungu na awaperekiwe kuwasaidiya wanu waja kuvushiwa?

2

Nafasi ulu yakuvushiwa

¹ Ndimana, tijuji titengemane tifulate pakulu vyatisikira ipate tisipoteye.

² Kamana habari zereziwe na malaika zoloka, watúpa shariya onse na wabishi wapata hukumu iwajúzure ³ Kwa javyo, futi ofwe ikiwa atiyeriwa tisaka kunusurikaja na kuvushiwa kukulu-ko? Kuvushiwa-ko ndi kwanzire kwereziwa na Mwenye mwaneyewe, ikisa wasikire watakikisha kuwa kweli.

⁴ Mwenyezimungu neye novyo ázidi kwakikisha kuwa habari-zo zakweli julu ya alama, matajabisa, maajuza a uwezo jisijisi, na julu yakutisusira uwezo wa Roho Takatifu, sawa-sawa na vyaasaka mwaneyewe.

Insa Almasihi áfungula njira tivushiwe

⁵ Mwenyezimungu aawapere malaika uwezo wakutawala ulumwengu mupya* watamba-wu. ⁶ Fala mMandiko Matakatifu mamojawapo† kalavya ushahidi javi:

“Yarabi Mwenyezimungu,
binadamu nani wakummwaza?

† **1:8** Ona Zaburi 45:6,7. ‡ **1:10** Ona Zaburi 102:25-27. § **1:13** Ona Zaburi 110:1. * **2:5**

Ulumwengu mupya ndi namuna nyengine zawaja kuinshi wenye kuvushiwa na Insa. † **2:6** Zaburi 8:4-6.

Binadamu akuyeri kakinani?

⁷ Kuntula utoto aba kawa sini ya malaika, kunkonga lemba ra utukufu na inshima,

⁸ kutula piya sini ya kumaulu kwake.”

Sambi, payambiwa kuwa “kutula piya sini yake”, mana ake ndi kuwa acipo anta kimoja saciri sini yake. Fala sambi-pa wanu atiri kuwawona piya sini yake.

⁹ Ila tankummona iye kuwa, kwa wakati aba, kâturiwa utoto koliko malaika. Iye Insa ndi ayerere kifo, julu ya rehema ya Mwenyezimungu, kwa ajili ya wanu piya. Ingawa kâturiwa utoto, fala sambi-pa, kwa sababu ya kutabika ka kifo, iye kakongiwa lemba ra utukufu na swifa!

¹⁰ Kamana iwapo shariya kuwa Mwenyezimungu, mwenyé vinu piya na mwenyé kumba piya, aje nawo wafulati wengi wawe upande wa utukufu wake. Katenda javyo julu ya kunteza Insa, awalóngoza wanu kuwavusha, awe kamilifu julu ya kutabika. ¹¹ Kamana ire atakátifu, na ware watakatífiwa, walawirira ka Baba mmoja. Ndimana Insa aawona haya kuweta “wanduzangu”, ¹² kamba vyayambiwe mMandiko†:

“Níwerezwa baina vyautendanga uwe wanduzangu. Nukwimba nukukusifu mbere ya wanu wako.”

¹³ Mmandiko mengine, iye kaamba javi§:

“Omi níntumaini Mwenyezimungu.”

Ikisa kaamba tena:

“Niwa epa, na ware Mwenyezimungu waunaminire kuwasunga, ewo wawa kamba wanangu.”

¹⁴ Sambi, ware wetiwe wanawe na Insa, kwa kuwa ewo binadamu*, iye mwaneyewe kâlawirira kwa namuna moja ipate julu ya kifo cake, anshinde ire ári na uwezo wa kifo, Ibilisi. ¹⁵ Kwa namuna-yo, piya wákiwa watwana kwa milele kwa sababu ya kopa kufwa, Insa kawanusuru. ¹⁶ Kamana vikwijiwikana kuwa aajire kuwasaidiya malaika, ila kâja kusaidiya ujukulu wa Ibrahima. ¹⁷ Ndimana neye akijuzi awe sawa-sawa na wanduze kwa kila namuna, ipate awe nlongozi nkulu wa dini wakuwa ndi mwenyé huruma na mwaminifu. Kwa namuna-yo, antumike Mwenyezimungu, iye mwaneyewe awe kafara, ipate madambi a wanu aswamiwe. ¹⁸ Kamana, kwa kuwa katabika julu ya kushetwaniwa, iye kanawo uwezo wa kuwasaidiya ware wenye kushetwaniwa.

3

Insa ndi nkulu zaida ya Musa

¹ Kwa javyo umwe, wanduzangu watakatifu, wenzangu titiwe mbinguni, akuyerini Insa. Iye ndi walii na nlongozi wetu nkulu wa dini yatiri kwereza-yi. ² Kamba Musa vyaákiwa mwaminifu na kazi yake nnyumba ya

† **2:12** Ona Zaburi 22:22. § **2:13** Ona Izaya 8:17. * **2:14** Kigeregu: “wanawo nyama na damu”.

Mwenyezimungu^{*}, na Insa ákiwa mwaminifu ka Mwenyezimungu mwenyé kuntondola. ³ Musa kasifiwa, fala Insa kawoniwa kuwa ndi wakujúzi kusifiwa pakulu zaida ya iye, kamba njengi wa nyumba vyaasifiwa pakulu koliko nyumba yawenye. ⁴ Kamana kila nyumba ítengeziwa na munu, ila atengéza vinu piya Mwenyezimungu. ⁵ Musa ákiwa ntumisi mwaminifu nnyumba ya Mwenyezimungu piya, kalavya ushahidi wa vire víkija kwereziwa mbere. ⁶ Fala Insa Almasihi mwaminifu kamba mwana, amiri wa nyumba-yo. Na nyumba-yo ndufwe, ikiwa tizídi koloka mpaka mwinsho, na hakika na kwamini nkati ya tamaa yatirindira.

Ukosofu wa kutowa kwamini

⁷ Kwa javyo, kamba vyaamba Roho Takatifu† javi:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,
⁸ myoyo yenu musitaye ugumu,
 kamba wababu zenu pawábishane nami,
 suku yawániyerere nlanga.

⁹ Emo wababu zenu wániyerera waniwone canikisaka kutenda,
 ingawa wáwona vyaniwasaidiye muda wa myaka arubaini.

¹⁰ Ndimana níkimiwa na noco kizazi-co, níkisowera javi:
 ‘Daima wankukosa mmyoyo mwawo,
 wakatala kifulata njira zangu.’

¹¹ Kamba vyanílapire paníkimiwe, níkamba:
 ‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’ ”

¹² Wanduzangu, more-more asilawirire munu nkati yenu wakuwa na moyo mbaya wakutowa kwamini, wakulongoza kukatala kunfulata Nlungu hai. ¹³ Kwasa javyo, zidini kurimbisana myoyo kila suku sambu nopa pamwitiwe-pa, ipate asilawirire nkati yenu munu wakutaiwa moyo ngumu, wakuteseka na dambi. ¹⁴ Kamana kwamini kwetu katiwere nawo tangu mwanzo, tikizidi koloka mpaka mwinsho, tilawirira kuwa wenziwe Almasihi nkati ya kazi yake. ¹⁵ Ndi kamba vyayambiwe‡:

“Rero, mukisikira shauti ya Mwenyezimungu,
 myoyo yenu musitaye ugumu,
 kamba wababu zenu pawábishane nami.”

¹⁶ Epa wasikire shauti ya Mwenyezimungu wakibishana naye ndi wepi? Kusema kweli, sipiya walongoziwe na Musa kulawa Miswiri? ¹⁷ Na ware Mwenyezimungu waakimiyane nawo muda wa myaka arubaini ndi wepi? Siware wakorire dambi, wakifwira nlanga nomo? ¹⁸ Na paalapire kuwa “awaja kwingira mahala pangu papumuzi”, waakiwamba ndi wepi? Siware watupire kauli zake? ¹⁹ Basi, tereriwa kuwa awakidirire kwingira kwa sababu ya kutowa kutumaini.

4

¹ Kwa kuwa tanawo mpaka sambu-pa tamaa yakwingira mahala pake papumuzi, tiritunze sana-sana ipate asilawirire mmoja wenu wakusokerera kwingira nopo mahala-po. ² Kamana teréziwa Habari Ngema kamba

* **3:2** “Nnyumba ya Mwenyezimungu” mana ake “nkati ya Mwenyezimungu”. † **3:7** Ona Zaburi 95:7-11. ‡ **3:15** Ona Zaburi 95:7; Waebraniya 3:7.

vyawereziwe ewo^{*}, ila ewo cawasikire aciwafaire kinu, kwa kuwatowa umoja wa kwamini cawasikire. ³ Basi, ofwe wenye kwamini tingira nopo mahala papumuzi-po, kamba vyaâmbire Mwenyezimungu javi†:

“Kamba vyanilapire nkati ya nyongo yangu:
‘Awaja kwingira mahala pangu papumuzi.’”

Kasowera javyo ingawa kazi yake kâtimiza tangu pawisire kumbiwa ulumwengu. ⁴ Kamana kuhusu suku yasaba, nsitari mmoja wa Mandiko‡ ukwamba javi:

“Suku yasaba Mwenyezimungu kapumula kwa kutimiza kazi zake piya.”

⁵ Usowezi mmoja nowo uwiriziwa tena:

“Awashubutu kwingira mahala pangu papumuzi.”

⁶ Kwa kuwa wanzire kwereziwa Habari Ngema awengire kwa kutowa kusikiriza, wengine wapewa nafasi yakwingira nopo mahala papumuzi-po.

⁷ Tukwijiwa kinu kamba-ci konta Mwenyezimungu katula suku nyengine, kaamba kuwa ndi suku ya “rero” pairipo nafasi yakwingira mahala papumuzi-po. Kwa myaka mingi ipitire, Mwenyezimungu kâsowera julu ya Daudi, kamba vyaamba futi:

“Rero mukisikira shauti ya Mwenyezimungu, myoyo yenu musitaye ugumu.”

⁸ Kamana inawa Yoshwa wanu-wo kawalongoza mahala papumuzi, aikibidi Mwenyezimungu kusowera tena, kutula suku nyengine. ⁹ Kwa javyo, kamba Mwenyezimungu vyaapumure suku yasaba pesire kumba ulumwengu, ingaripo nafasi ya wanu wa Mwenyezimungu kupumula. ¹⁰ Kamana mwenyé kwingira mahala papumuzi pa Mwenyezimungu âpumula kazi zake sawa-sawa vyaapumure Mwenyezimungu kazi zake.

¹¹ Basi, mahala papumuzi-po, titende juhudi tingire, ipate asiwepo wakunkuna kamba vyaviwakunire mida, wakitowa kwingira kwa sababu ya ubishi.

¹² Kamana usemi wa Mwenyezimungu uwa nawo uhai na nguvu, unorêka pakulu kupunda jambiya yakusinja kuno na kuno. Úpitirira mpaka mmoyo, ukwawanya moyo na roho kamba jambiya vyayawanya nyama na makongolo. Ndimana usemi wa Mwenyezimungu úkidiri kwawanya mawazo meema na mabaya a mmoyo. ¹³ Aapo kiyumbe akidiri kufisa siiri mbere ya Mwenyezimungu. Kwake iye, piya viwa paweru, awona vinu piya na maso ake. Na vitendo vyatitenda tijuži kunjibu.

Insa atipendeleya mbere ya Mwenyezimungu

¹⁴ Sambu, kwa kuwa tanawo nkulungwa nkulu wa dini atangurire binguni, Insa, Mwana wa Mwenyezimungu§, tukeni tikore makono mawiri kwamini

* **4:2** “Ewo” ndi ware wâkiwa nlanga. † **4:3** Ona Zaburi 95:11. ‡ **4:4** Ona Mwanzo 2:2. § **4:14** “Mwana wa Mwenyezimungu” ndi zina rimojawapo retiwa Insa. Rikolota kupatana kwema ka Insa na Mwenyezimungu, kamba mwana na wawaye. Eri zina-ri aisema kuwa cipita kitendo ca muka na nlume, ila kupatana kukulu ka kiroho.

kwetu katereze. ¹⁵ Kamana nlongozi wetu nkulu wa dini akidiri kutiwonera utungu ufuko wetu, kwa kuwa kashetwaniwa kwa namuna-zi piya kamba vyatishetwaniwa ofwe, ila iye aakorire dambi. ¹⁶ Basi, tukeni na uhakika tiwe karibu na kiti ca Mwenyezimungu, tipate huruma na rehema patisakula kusaidiwa.

5

¹ Kila nkulu wa wakulungwa wa dini ákitondoriwa nkati ya wanu, ak-itawaziwa ipate antumike Mwenyezimungu kwa faida ya wanu. Kazi yake ikiwa yakupereka kafara na swadaka ipate wanu wafutiwe madambi awo. ² Watikínifu na sawári makamilifu, iye ákidiri kuwawonera utungu, kwa kuwa iye mwaneyewe kaveya. ³ Kwa javyo, ájuzi apereke kafara kwa madambi ake iye mwaneyewe kamba vyaalavya kafara kwa madambi a wanu wengine. ⁴ Na hapana munu wakuritawaza mwaneyewe cewo cakusi-fiwa-ci, ila akolotiwa na Mwenyezimungu kamba vyavínkunire Aruna.

⁵ Kwa namuna moja noyo, Almasihi aaritawaze iye mwaneyewe ub-ora wakuwa nkulungwa wa dini. Ila Mwenyezimungu kantondola, akimwambira*:

“Uwe kuwa mwanangu,
rero omi nukupongola.”

⁶ Na mahala pengine†, akwamba tena javi:

“Ukuwa nlongozi wa dini wa milele,
kamba vyaawere Melkizideki.”

⁷ Insa, mainsha ake mulumwengu-mu, akilebelanga duwa ka Mwenyezimungu, mwenyé uwezo wakunvusha nkati ya kifo. Akilebelanga kwa shauti ulu-ulu kuno akinlawa masozi. Na akisikiriziwa kwa sababu ya kunyenyekeya kwake kutenda vyaasaka Mwenyezimungu. ⁸ Ingawa ákiwa mwana, karifunda kutwii julu ya tabu zimpatire. ⁹ Na paatimize vinlazimire kutenda, kalawirira kuwa Nvushi wa milele wa piya wenye kunfulata. ¹⁰ Na Mwenyezimungu kantula kuwa nkulu wa wakulungwa wa dini, kwa namuna moja noyo kamba vyaákiwa Melkizideki.

Usase kuntumaini Insa Almasihi

¹¹ Kuhusu ewu mwaha-wu‡, tanawo vinu vingi vyawenye vyakukwerezani. Fala virigariga kukwerezani konta amusaka kwereriwa. ¹² Kamana, ingawa upita wakati mwingi, mujuzi muwe wanlimu, fala munsakula munu akufundeni vinu vyakwanza vya habari za Mwenyezimungu. Muwa kamba watoto musakula kujiji maziwa, iri hali mukijuzi murye cakurya cakukamatiwa. ¹³ Kamana ájuzi kunywa maziwa onse angari toto, ndi sejiwa cema. ¹⁴ Fala cakurya cakukamatiwa ndi cankulungwa. Kwa njira ya kufundiwa, ewo wanawo ankili yakutondola cema na kibaya.

* 5:5 Ona Zaburi 2:7. † 5:6 Ona Zaburi 110:4. ‡ 5:11 “Mwaha-wu” ndi kuwa Almasihi vyaawere nkulungwa wa dini kamba vyaákiwa Melkizideki.

6

¹ Kwa javyo, tase vyatanzire kurifunda kuhusu Almasihi, tukeni mbere mpaka tifikirire vyakurifunda vyakukamilika. Tisijenge tena upya aliserusu zakufulata ngano kamba ezi:

cakwanza, ibidi kutubiya vitendo vyakuja na kifo, na kurimbirira kuntu-maini Mwenyezimungu;

² capiri, kufunda kuhusu koza, alama ya kutubiya; catatu, kuntula munu makono; caane, kuwafufula wanu ka wafwi; na catanu, kulamuriwa ka milele.

³ Nevyo, Mwenyezimungu akisaka, títenda.

⁴ Kamana ware wasire kunkubali Insa, aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena upya. Ewo mara moja wâpokerera nuru ya Mwenyezimungu, wâyeza thawabu ya binguni, wâpokerera Roho Takatifu pamoja na wenzi-wawo. ⁵ Wâyerera wema wa usemi wa Mwenyezimungu, na wâyerera vitendo vya uwezo visaka kukuna paa kutawala Mwenyezimungu. ⁶ Fala novyo-sivyo, wantula minyongo iye! Aapo akidiri kuwaludisira kutubiya tena, konta wankejeli baina Mwana wa Mwenyezimungu, wangomezera tena mpaka warihukumu.

⁷ Kamana ewo wawa kamba ardhi inywa maji a nvula painya ponse. Ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya kuwafâi warimi, ardhi-yo ijanliiwa na Mwenyezimungu. ⁸ Fala ikiwa ardhi-yo iruwerya miti ya miwa na mbiriwiri, saifâi na karibu yakulaniwa. Ardhi-yo mwinshoni ikociwa.

⁹ Wapendani wangu, ingawa tisowera javi, titumaini kuwa umwe mwanawo vinu vyema pakulu, vyakuja na kuvushiwa. ¹⁰ Kamana Mwenyezimungu ndi mwenyê shariya, akwijiwa camutenda, na namuna vyamuwapenda wenzenu kwa zina rake, pamuwasaidiya watakatifu, na mpaka sambipa mungari kutenda novyo. ¹¹ Vitajibu pakulu kuwa umwe-po kila mmoja olote juhudi moja mpaka mwinsho, ipate muwe na uhakika wa tamaa yamurindira na imani. ¹² Nkati ya kwamini kwenu, musiwe wafuko, ila muwafulatize ware warîti tamaa julu ya kutumaini na imani.

Mwenyezimungu atimiza tamaa yake

¹³ Mwenyezimungu, paampere tamaa Iburahima, kârilapira mwaneyewe kuwa atimiza tamaa yake, konta aawerepo mwengine wakunzaidi iye. ¹⁴ Iye kaamba*:

“Nilapa ka ukweli kuwa uwe nukujanliya pakulu, nukupa ujukulu mwingi wawenye.”

¹⁵ Ndimana Iburahima, kwa kuwa akirindira na imani, tamaa ire akipata.

¹⁶ Munu paalapa, anlapira munu wakunzaidi álavya ushahidi, na kilapo ciwalavya wanu dana. ¹⁷ Basi, Mwenyezimungu kâsaka kuwa ware waja kuriti tamaa yake wejiwe kuwa aapindula vyaasemire, ndimana tamaa-yo iye kalapira. ¹⁸ Kwa javyo, julu ya vinu viwiri† savipinduriye, (na novyo avikidirika Mwenyezimungu kulongopa), ofwe tintuwirire iye tirimbisiwa myoyo tikore makono mawiri tamaa ituriwe mbere yetu. ¹⁹ Eyo tamaa-yo iwa kamba nanga ya ngalawa, ítirimbisa myoyo isive na dana isaka kuwa yonse. Kamana tamaa-yo ípita papazira ya nyumba takatifu ya mbinguni,

* **6:14** Ona Mwanzo 22:17. † **6:18** “Vinu viwiri” ndi tamaa yaalavire Mwenyezimungu na kulapa kwake.

ikwingira mahala patukufu paari Mwenyezimungu. ²⁰ Kweli, epo ndi pengire Insa, kábula ya ofwe, kwa ajili yetu. Kamba vyaawere Melkizideki, neye novyo kalawirira kuwa nkulungwa wa dini wa daima milele.

7

Melkizideki nlongozi wa dini

¹ Noyu Melkizideki-yu ákiwa nfalume wa Salemu, na ákiwa nlongozi wa dini akintumika Mwenyezimungu, Nlungu nkulu pakulu. Iye paakiludi Iburahima kuvita yakuwashinda mafalume, kasimanana naye, akinjanliya.* ² Iburahima, vinu piya vyâapatire kuvita, kálavya fungu rakumi, akimpa Melkizideki. Zina ra Melkizideki mana ake “nfalume wa shariya”. Kwa kuwa ákiwa nfalume wa Salemu, zina rake rikiwa nawo novyo mana ake “nfalume wa usalama”. ³ Iye aawere nawo wawaye wala mamaye, wala aipo waraka ya mazina a wakinya babuze. Ejiwikane mwaka waapongoriwe wala waafwire. Ndimana akilandanisiwa Mwana wa Mwenyezimungu, kawa nlongozi wa dini wa milele.

⁴ Onani, Melkizideki vyawere munu bora pakulu! Anta Iburahima, noyo babu yetu nkulu, kâmpa fungu rakumi kwa vinu vyaawapokere maadui wake kuvita. ⁵ Na ujukulu wa Lawi, ware wâpewe cewo ca ulongozi wa dini, watumiwe nTaureti kupokerera fungu rakumi ra vinu vyawakipatanga wanu waIzraeli, wanduzawo, ingawa newo novyo wákiwa ujukulu wa Iburahima. ⁶ Basi Melkizideki, ingawa aawere wa rikolo ra Lawi, kâpokerera fungu rakumi ra Iburahima, na kânjanliya Iburahima, noyo âpokere tamaa za Mwenyezimungu-yo. ⁷ Hapana atikina kuwa ire ajanlíya ndi bora koliko ajanlíya. ⁸ Kwa upande wa walongozi wa dini wa rikolo ra Lawi, wâpokerere fungu rakumi wákiwa wanadamu mwinsho wafwa. Fala upande wa Melkizideki, ripokereriwa na munu ari hai, kamba vyaaulaviwe ushahidi kuhusu iye. ⁹ Tanawo shariya ya kwamba anta Lawi, akipokereranga fungu rakumi noyo, neye novyo kalavya fungu rakumi julu ya Iburahima, ¹⁰ kwa kuwa ákiwa mmwiri mwa Iburahima babuye, paasimanane na Melkizideki.†

Nlongozi mwengine wa dini, kamba Melkizideki

¹¹ Sambu, íkisakikana kazi ya walongozi wa dini wa rikolo ra Lawi ipate wanu wa Izraeli wafulate shariya yawâpewe. Ináwa ulongozi-wo utimiza ukamilifu, singari kasakikana nlongozi wa dini wa namuna nyengine kamba Melkizideki, sairi wa namuna ya Aruna wa rikolo ra Lawi. ¹² Paatawaziwa nlongozi mwengine wa dini, ilazimu shariya neyo novyo ipinduriwe.† ¹³ Kamana Mwenye wetu, ambíwa mMandiko-mu, aawere wa rikolo ra Lawi, na nkati ya rikolo rake tangu aalawirire mmojawapo wakutumika cewo ca nlongozi wa dini.Š. ¹⁴ Aapo atikina kuwa Mwenye wetu kálawirira kurikolo ra Yuda. Na kuhusu rikolo-ro, Musa aasowere kinu upande wa nlongozi wa dini.

¹⁵ Sambu tikwereriwa sana: kálawirira nlongozi wa dini namuna nyengine, wakulandana na Melkizideki. ¹⁶ Iye aalawirire kuwa nlongozi wa dini kwa kufulata shariya na shuruti za kufulatana ka rikolo, ila kwa sababu

* **7:1** Ona Mwanzo 14:17-19. † **7:10** Kusema kweli, nowo wakati-wo Lawi ákiwa saanapongoriwa.

† **7:12** Shariya isema nani ári na haki yakuwa nlongozi wa dini. § **7:13** Kigeregu: “uralu”.

ya uwezo wa mainsha ake seesa tena. ¹⁷ Kweli, Mandiko Matakatifu* akwamba:

“Uwe kuwa nlongozi wa dini wa milele kwa namuna ya Melkizideki.”

¹⁸ Basi shuruti ya mida yasiwa konta aina nguvu na aifāi kinu, ¹⁹ kamana Taureti aifikamilisha kinu. Fala sambi-pa Mwenyezimungu katisakurira tamaa ngema pakulu ipate julu yake tiwe pamoja naye.

²⁰ Na eyi tamaa-yi yakikishiwa kwa kilapo. Pawakitawaziwa walongozi wa dini wengine, Mwenyezimungu aalapire, ²¹ fala paalawirire eyu kuwa nlongozi wa dini, Mwenyezimungu kalapa, kamwambira javi†:

“Omi Mola nīlapa, sipindula kauli yangu. Ukuwa nlongozi wa dini wa milele.”

²² Kwa sababu ya kilapo-co, Insa atipa uhakika kuwa eyi miyadi-yi ndi bora pakulu zaida ya mida.

²³ Visitoshe, mida wākiwapo walongozi wa dini wengi wakorire kazi fala mwinsho wafwa, awakidirire kuzidi kukola kazi. ²⁴ Fala Insa kankuinshi kwa milele, na kazi yake ya ulongozi wa dini saupitaniwa tena. ²⁵ Kwa javyo, iye kanawo uwezo, sambi-pa mpaka milele, wakuwavusha wanu wōka ka Mwenyezimungu julu yake. Kweli, iye kankuinshi daima-zi kuno akiwalebelela nowo wanu-wo.

²⁶ Basi Insa ndi nkulu wa wakulungwa wa dini wakutitendera piya visakikana vyonse. Iye takatifu, aana dambi anta mmoja wala kinu cakunyata, na katanusiwa nkati ya madambi mulumwengu-mu akituriwa mbinguni. ²⁷ Iye aari kamba walongozi wa dini wa mida, wakiperekanga kafara daima-zi, cakwanza wakitenda wapate kufutiwa madambi awo wanyewe, ikisa ka madambi a wenzawo. Fala ka Insa sijavyo! Iye, paaripereke mwananyewe, kalavya kafara mara moja noyo tu basi kwa daima. ²⁸ Nkati ya Taureti, wanu sawakiwa makamilifu wakitawaziwanga kuwa walongozi wa dini. Fala kauli ya kilapo, cilapiwe bandi ya Taureti, katawaziwa Mwanawe, mwenyé kukamilika daima milele.

8

Insa ndi shikarakanzi wa miyadi yanguvu pakulu

¹ Onani, kinu maalumu catiri kwamba ndi kuwa tanawo nkulungwa nkulu wa dini wa namuna-yo, ekare nkono nriri wa kiti ca Mwenye Nkulu mbinguni. ² Iye áhudumu vitakatifu nkati ya ema takatifu yakweli, saitengiwe na wanadamu, ila Mola. ³ Kila nkulungwa nkulu wa dini ákitondoriwa apereke swadaka na kafara. Ndimana ikilazimu neye awe nawo kinu kimojawapo cakupereka. ⁴ Insa, anawepo mulumwengu-mu, aangari kuwa nlongozi wa dini, konta kuno wawapo walongozi wa dini waperéka kafara na swadaka, kamba vyaishurutisa Taureti. ⁵ Kazi zawatenda ewo nfano tu basi au kinviri ca kazi zitendiwa mbinguni. Kwa sababu ya javyo, Musa paawere tayari kujenga ema ya miyadi ya kupatana, kámbeririwa na Mwenyezimungu javi: “More-more, utende sawa-sawa kamba nfano vyawoloteriwe kumwango.”

* 7:17 Ona Zaburi 110:4. † 7:21 Ona Zaburi 110:4.

⁶ Fala sambi-pa, Insa kagabiziwa kazi bora pakulu koliko wakulungwa wa dini wa mida, kwa kuwa iye ndi mwenyé kupatanisa kwa miyadi bora pakulu ya kupatana. Ndi javyo konta miyadi-yo yanawo tamaa bora pakulu.
⁷ Kamana miyadi ya kupatana yakwanza, ínawa íkamilika, aikisakikana kutula miyadi myengine ya kupatana kapiri.

⁸ Fala mMandiko Matakatifu*, Mwenyezimungu áwasutumumu wanu wake javi:

“Wakati uwa karibu wanija kutula miyadi mipya ya kupatana, na wanu wa Iziraeli pamoja na wanu wa rikolo ra Yuda.

⁹ Eyo miyadi mipya-yo aija kuwa kamba yanitirire mida na wababu zawo, paníwalongoze sana-sana, nikiwalavya Miswiri.

Ewo awafulate kamba vyaikisaka miyadi-yo, ndimana awanierire, amba ndi Mola.

¹⁰ Basi, eyo ndi miyadi yanjá kutula na wanu wa Iziraeli bandi ya nozo suku-zo, amba ndi Mola.

Shariya zangu nitula nkati ya mawazo awo, nikwandika mmyoyo mwawo.

Omi nukuwa Nlungu wawo, newo wakuwa wanu wangu.

¹¹ Aashubutu munu kufundana na mwenziwe wala kufundana na nduye, kumwambira: ‘Mwijiwe Mola’, konta piya-wo wakuja kunijiwa, ntoto kamba nkulu.

¹² Nukuja kuwatendera huruma, kuswamii makosa awo, madambi awo sishubutu kukumbukira tena.”

¹³ Mwenyezimungu paambire miyadi mipya, miyadi yakwanza katula kuwa yuluvala. Na kinu culuware na cisire ciwa karibu yakwasiwa kutu-miriwa.

9

Miyadi mipya kwa damu ya Insa

¹ Sambu, kwa kutimiza miyadi yakwanza, wanu wakijuzi wantukuze Mwenyezimungu kwa kufulata shariya zituriwe. Na wakiwa nawo novyo mahala patakatifu mulumwengu-mu, ² Ema Takatifu ítengiwa. Ikiwa na misana miwiri. Nsana wakwanza wakwingirira úkitiwa “Mahala Patakatifu”. Nkati-mo múkiwa kandiyeru, meza, pamoja na mikate takatifu*. ³ Noyo ema-yo nkati-mo ilumuriwa na pazira. Nkati ya pazira-yo, nsana mwengine úkitiwa “Mahala Patakatifu Pakulu”. ⁴ Nopo ndi paukiwa uralu wakupambiwa na oru, na “Kashoti ya Miyadi” upande piya wakupambiwa na oru. Nkashoti-mo cikiwapo kiyungu ca oru citaiwa maná, ngombo ya Aruna yaásipuse Mwenyezimungu, pamoja na maluwawo mawiri a mawe ándikiwe áhuri za Mwenyezimungu. ⁵ Julu ya kashoti-yo, víhuriwa nfano viyumbé vya utukufu. Mbawa zawo zakukunjuka zífinika mahala Mwenyezimungu pakiswamii madambi. Kuhusu novi vinu-vi, aipo nafasi sambi-pa yakwereza piya.

* 8:8 Ona Yeremiya 31:31-34.

* 9:2 Mikate takatifu ikilaviwanga swadaka ka Mwenyezimungu.

⁶ Piya-vi pavitengeziwe sana-sana, walongozi wa dini wakingiranga nsana wakwanza wa ema[†] wakitenda kazi zawo. ⁷ Fala nsana wapiri wa ema[‡], nkulu wa wakulungwa wa dini iye tu basi ndi akingira. Visitoshe, akingira kila mwaka mara moja basi, akisukula damu ya kafara akapereke ka Mwenyezimungu, anlebele aswamii madambi ake na madambi awakorire wanu kwa sababu ya kutikina. ⁸ Kwa piya-vi, Roho Takatifu átolotera kuwa, ikiwa ema ya miyadi ya mida ingari kutumika, ilanda kuwa njira yúka Mahala Patakatifu Pakulu ainafunguriwa. ⁹ Piya-vi kinyume, namuna yakutifunda vinu vya faida rero-vi. Mana ake ndi kuwa swadaka na kafara za manyama zikilaviwanga ka Mwenyezimungu zire azikidirire kukamilisha myoyo ya wanu wakilavyanga kafara wawenye-wo. ¹⁰ Ezi kafara na swadaka zitendiwa-zi zishugulikira vinu vya mwiri basi, kwa nfano, namuna ya kurya, kunyua, na zakuriswafi. Zitumika mpaka Mwenyezimungu paasaka kutula namuna nyipya za kuinshi.

¹¹ Fala Almasihi, paalawirire kuwa nkulu wa wakulungwa wa dini kuwa atipe vyema vyaajsire, iye kawa ema bora pakulu na yakukamilika kupunda ikiwepo mulumwengu-mu. Ema-yo aitendiwe na wanadamu, mana ake siyo ya mulumwengu-mu. ¹² Iye, pengire mara moja tu basi kwa milele Mahala Patakatifu Pakulu, aasukure damu ya mbuzi wala ya ng'ombe ila kásukula damu yake iye mwaneyewe, apate kutombola milele. ¹³ Mida wanu wacafu miri yawo ikiswafiwa julu ya kutawanyika damu ya mbuzi au ya ng'ombe, na kúpakiwa rivu ra mwana wa ng'ombe wakociwa. ¹⁴ Kwa javyo, futi damu ya Almasihi aizidi kutiswafi? Iye, julu ya Roho wa milele, karipereka mwaneyewe kawa kafara kamili saina baka ka Mwenyezimungu. Damu yake itiswafi myoyo yetu, tase vitendo vitilongoza kukifo, ipate tintumike Nlungu hai.

¹⁵ Kwa javyo, Insa Almasihi ndi mwenyé kupatanisa kwa miyadi mipya, ipate irati ya milele Mwenyezimungu yaawapere tamaa ware watondoriwe wapate. Iwapo eyi nafasi-yi konta madambi awo awakorire wakati wa miyadi ya mida womboriwa na kifo ca Almasihi. ¹⁶ Sambu, miyadi yakupatana yaaturire Mwenyezimungu iwa kamba waraka yakuritisa. Upande wa noyi waraka-yi, ikibidi kwakikishiwa mwenyé kwandika-yo kuwa kafwa. ¹⁷ Kweli, waraka yakuritisa aina faida ikiwa andike-yo angari hai, fala bandi ya kufwa andike, waraka-yo yanawo faida. ¹⁸ Ndimana ikibidi kuwa ciwepo kifo kimojawapo ipate miyadi iwe na faida. Anta miyadi yakwanza, noyo aitimike bila kutawanyika damu. ¹⁹ Mmiyadi yakwanza, Musa pesire kuwambira wanu piya ámuri ya nTaureti, kátumira minyani ya husopo yakufungiwa na luzi reundu, kátwala damu ya ng'ombe na ya mbuzi. Ikisa akisulusa na maji, akisasanyira kitabu ca Taureti pamoja na wanu piya, ²⁰ akamba§: “Eyi ndi damu ya miyadi yaaturire Mwenyezimungu kwenu unwe.” ²¹ Na ema ya miyadi-yo, pamoja na piya vinu vikitumiriwa nkati yakuntukuza Mwenyezimungu, Musa kásasanyira novyo damu. ²² Basi, Taureti ikilazimisha kiyasi ca vinu piya viswafiwe julu ya kutawanyika damu. Na ikiwa damu aitawanyike, akupo kuswamiwa dambi.

²³ Sambu, ikibidi kuwa vyombo vikitumiriwa kuntukuza Mwenyezimungu viswafiwe julu ya namuna-yi. Fala evyo mifano tu basi ya vinu vyakweli viri mbinguni. Ndimana vinu vyakweli mbinguni vishurutisa kafara ya faida

† 9:6 “Nsana wakwanza wa ema” ndi “Mahala Patakatifu”. ‡ 9:7 “Nsana wapiri wa ema” ndi “Mahala Patakatifu Pakulu”. § 9:20 Ona Kulawa 24:8.

bora pakulu. ²⁴ Kamana Almasihi engire Mahala Patakatifu pakutendiwa na makono a wanadamu, engire pakulandanisiwa nfano tu basi wa mahala pakweli. Aiwere javyo! Kêngira mbinguni kawenye, mbere ya Mwenyezimungu, kutitendera fadili ofwe. ²⁵ Na engire kurilavya kafara mara nyingi, kamba nkulungwa wa dini wa Mayahudi vyakingiranga Mahala Patakatifu Pakulu kila mwaka, na damu sairi yake. ²⁶ Inawa javyo, Almasihi akijuzi atabike mara nyingi zawenye tangu kumbiwa ka ulumwengu. Kwasa javyo, epa utimizwa wakati wa mida, ufika wakati wa sambu-wu, iye kolotiwa kwa kuripereka kufwa mara moja tu basi kwa milele, alavye mizigo ya dambi. ²⁷ Piya wanu ituriwa wafwe mara moja tu basi, ikisa waje walamuriwe na Mwenyezimungu. ²⁸ Kwa javyo Almasihi, neye novyo kâripereka mara moja kuwa kafara alavye dambi za wanu wengi. Ikisa, akúja kwisuka mulumwengu mara yapiri, fala eyo mara-yo, anzima yake siyo kulavya dambi, ila kuwavusha wanu wari kurrindira iye.

10

¹ Kwa kifulata Taureti, wanu wakisaka kuka karibu ya Mwenyezimungu kuntukuzwa wakilavya kafara daima-zi kila mwaka. Fala Taureti tangu-tangu aiwere na uwezo wa kuwaswafi wanu-wo. ² Ináwa nowo wanu-wo kweli-kwelinini waswafiwa nfululu, awangari kurifahamu tena kuwa na madambi, ndimana singari isakikana kuludira tena kutenda kafara, sinovyo? ³ Fala kusema kweli, nozo kafara-zo zankuwatenza wanu kukumbukira dambi zawo kila mwaka. ⁴ Konta damu ya ng'ombe na ya mbuzi aina uwezo wa kulavya dambi.

⁵ Kwa javyo, Almasihi, pengire mulumwengu-mu, kasema ka Mwenyezimungu*:

“Ausakire kafara wala swadaka, ila kunitengeza mwiri.

⁶ Azukwajibu kafara za nyama wakociwa, wala swadaka ipate uswamii madambi.”

⁷ Ikisa Almasihi kamwambira Mwenyezimungu:

“He Mwenyezimungu, niwa epa kutimiza nafsi yako, kamba vyavyandikiwe kuhusu omi nkitabu ca Mandiko.”

⁸ Basi Almasihi, bandi yakusema:

“Ausakire na azukwajibu kafara za manyama wakociwa, wala swadaka zakulaviwa kupata kuswamiwa madambi”

(ingawa ezi kafara-zi zilazimishiwa nkati ya Taureti), ⁹ kamwambira Mwenyezimungu: “Niwa epa kutimiza nafsi yako.” Basi, Almasihi kafuja miyadi ya mida† katula miyadi yapiri‡. ¹⁰ Kwa noyo nafsi-yo, julu ya swadaka ya mwiri wa Insa Almasihi mara moja kwa milele, ofwe titakati-fwa.

* **10:5** Ona Zaburi 40:6-8. † **10:9** Kafuja miyadi ya mida pamoja na tabiya yakulavya kafara-yo.

‡ **10:9** “Miyadi yapiri” ndi kafara nyipya ya Insa mwaneyewe.

¹¹ Kila nlongozi wa dini awahudumu Mayahudi kila suku ákikola kazi, ákipereka kafara namuna moja noyo mara nyingi zawenye. ¹² Falakini Almasihi kârilavya iye mwaneyewe akiripereka kuwa kafara kwa mara moja noyo tu basi, kafara-yo ifâi milele. Ikisa kekala mahala bora pakulu, upande wa nkono nriri wa Mwenyezimungu. § ¹³ Tangu nopo kankurinda mpaka Mwenyezimungu awature maaduwi wake kumaulu kwake.* ¹⁴ Basi iye, kwa kuripereka mara moja noyo tu basi, ware waawatenza utakatifu kawatula ukamilifu kwa milele. ¹⁵ Na kinu-ci Roho Takatifu neye katakikisha, kanza kutereza usemi wa Mola asema javi†:

¹⁶ “Bandi ya nozo suku-zo, eyi ndi miyadi yanija kuwaturira ewo, amba ndi Mola. Shariya zangu nitula mmyoyo mwawo, nikwandika nkati ya mawazo awo.”

¹⁷ Ikisa kaamba javi‡:

“Madambi awo na makosa awo sishubutu kukumbukira tena.”

¹⁸ Onani, madambi-yo paaswamiwe, aisakikana tena swadaka nyengine yakufuta.

Tukeni tiwe karibu ya Mwenyezimungu

¹⁹ Sambu, wanduzangu, tanawo uhakika wakwingira Mahala Patakatifu Pakulu julu ya damu ya Insa, ²⁰ njira nyipya ya uhai katifungurira julu ya kupapula pazira paapereke mwiri wake. ²¹ Ndi kweli novyo kuwa tanawo nlongozi wa dini nkulu pakulu, amiri wa nyumba ya Mwenyezimungu mbinguni. ²² Kwa javyo, tukeni tiwe karibu ya Mwenyezimungu na myoyo ya ukweli na kwamini nfululu, tiwe na myoyo yakosiwa fahamu mbaya na miri yetu yakoziwa na maji swafi. ²³ Tamaa yatereziwe, tukeni tizidi kutumaini bila dana, konta Mwenyezimungu alavire tamaa mwaminifu.

²⁴ Tukeni tiwaze namuna zakushongana pendo na vitendo vyema. ²⁵ Tisitowe, kamba tabiya za wanu wamojawapo, kuka kujumana na wenzetu kujamati. Kwasa javyo, tukeni tirimbisane myoyo kila mara, konta mukwijiwa kuwa suku ya Kiyama iwa karibu.

²⁶ Kamana bandi yakwereriwa ukweli sana-sana na kukubali, tikilangela kuzidi kukola dambi, basi aipo kafara anta moja yakufâi kutiswamii madambi. ²⁷ Ila ka wabishi, ciwabakire kinu kimoja basi, kurindira na wofi nkulu hukumu ya Mwenyezimungu na kulungula moto mwingi wakofya.

²⁸ Mida mnu akikatala kufulata Taureti yésusiriwe Musa, wakilawirira mashahidi wawiri wakwakikisha kuwa kakosa akihukumiwa kifo, aakiwoneriwa utungu. ²⁹ Fikirini ndi hukumuni ulu iwapata wanu wakunkejeli Mwana wa Mwenyezimungu! Ware sawatula ubora damu ya Insa yakwakikisha miyadi ya kupatana iswamii dambi yake! Novyo, wakejeli damu ya miyadi itiswafire, na wafezeyi Roho Takatifu atolotera rehema!

³⁰ Kamana tikwijiwa kuwa Mwenyezimungu nkati ya Mandiko Matakatifu § kaamba javi:

§ **10:12** Ona Zaburi 110:1. * **10:13** Ona Zaburi 110:1. † **10:15** Ona Yeremiya 31:33. ‡ **10:17** Ona Yeremiya 31:34. § **10:30** Ona Kumbukumbu 32:35-36.

“Kuriripira kwangu; omi niriripirira.”

Na mahala pengine mMandiko, yandikiwa javi:
“Mola awalamula wanu wake.”

³¹ Kugwirira makono mwa Nlungu hai ndi kinu cakofya pakulu!

³² Wazani suku zipitire bandi yakupata nuru ya Mwenyezimungu, muhitamili tabu nyingi zawenye. ³³ Umwe kati yenu, wamojawapo watukaniwa pawanu na watabishiwa, na wengine wakisanganyika na watabishiware, newo novyo watabika. ³⁴ Mutabika pamoja na wafungwa, na pavitariwe vinu vyenu piya, muhitamili hasara na furaha, kwa kuwa mukijiwa kuwa mukuja kupata vyema pakulu vyakuwepo daima. ³⁵ Basi, musase kurimba moyo konta kukujisirani tuzo rikulu. ³⁶ Kamana mujuzi muhitamili kwa imani mutimize nafsi ya Mwenyezimungu, ipate mupokerere vire vyaakupereni tamaa. ³⁷ Konta mMandiko*, Mwenyezimungu akwamba:

“Ubaki wakati aba futi wakuja ire akirindiriwa, aakáwa.

³⁸ Fala kamilifu wangu áinshi julu ya kwamini†. Saanihitamili, siri radi naye.”

³⁹ Ofwe atiri kamba ware sawahitamili wakupoteya, ila tintumaini Mwenyezimungu, ndimana tivushiwa.

11

Namuna zakuntumaini Mwenyezimungu

¹ Sambi, “kwamini” mana ake ndi kuwa nawo uhakika wakuwa na tamaa ya vinu saviwoneka viri vyakweli. ² Kamana julu ya kwamini, wababu zetu wa mida wajibisa ka Mwenyezimungu.

³ Julu ya kwamini, tikwereriwa kuwa wasaa umbiwa julu ya usemi wa Mwenyezimungu, vinu vyakuwoneka vyumbiwa na kinu saciwoneka.

⁴ Julu ya kwamini, Abeli kalavya kafara ngema zaida ya Kaini, ndimana kajibisa ka Mwenyezimungu kuwa kamilifu. Mwenyezimungu kolota kuwa kawa radi naye julu yakupokerera kafara yake. Ingawa iye káfwa, fala julu ya kwamini kwake, angari akisowera.

⁵ Julu ya kwamini, Henoki katwariwa kaperekiwa mbinguni, iye aafwire. Hapana munu ammonire tena konta Mwenyezimungu kantwala. Kábula yakutwariwa mulumwengu-mu, kâjibisa ka Mwenyezimungu. ⁶ Aashubutu munu kwajibisa ka Mwenyezimungu bila kuntumaini iye. Konta asakúla kuka upande wa Mwenyezimungu ájuzi atumaini kuwa iye kawapo na awatuzi wenye kuka upande wake.

⁷ Julu ya kwamini, Nnu kâsikiriza sana-sana paambiriwe na Mwenyezimungu kuhusu vinu savikiwoneka vikija kukuna mbere. Kwa kumwinshimu Mwenyezimungu, kalunda safina invushire iye pamoja na jamaa zake. Kwa namuna-yo, Nnu kâlamula kuwapa hukumu wanu wa mulumwengu-mu. Novyo, kâriti ukamilifu wakulawirira julu ya kwamini.

⁸ Julu ya kwamini, Ibrahama kâsikiriza paamuriwe kusama, kuka inti nyengine yaampere tamaa Mwenyezimungu kuwa akuja kuriti. Kôka ingawa aakijiwa mahala kaakuka.

* **10:37** Ona Habakuki 2:3. † **10:38** Ona Habakuki 2:4; waRoma 1:17; waGalata 3:11.

⁹ Julu ya kwamini, akiinshi kamba malamboni inti yaâmpere tamaa Mwenyezimungu. Iye ákikalanga muema pamoja na Izaki na Yankubu, wenye kuriti sawa-sawa cire caâwapere tamaa Mwenyezimungu. ¹⁰ Iburahima akirindira kwikala kaya ya aliserusu yakukomala, yaapangire na yaajengire Mwenyezimungu mwaneyewe.

¹¹ Julu ya kwamini, Iburahima kâpata uwezo wa kumpongola mwana. Ingawa kôluvala pakulu na nkawake Sara aakipongola, kâkidiri konta akitu-maini kuwa Mwenyezimungu kamilifu, atimiza tamaa yake. ¹² Kwa javyo, julu ya munu mmoja, noyo ári karibu kufwa, ulawirira ujukulu mwingi wawenye, kafyala-kafyala kamba nondwa za mbinguni au kamba misanga ya mwani.

¹³ Julu ya kwamini, ewa wanu-wa piya wafwa wakitumaini, bila kupata kinu cawapewe tamaa, fala mmoyo wakiwona na wakisheherekera baidi, na wakikisha kuwa inti ire aiwere yawo, ila ewo wanu wakupíta mulumwengu-mu. ¹⁴ Wakiséma javyo kolota kuwa wankusakula inti yawo wanyewe. ¹⁵ Inawa wakiwaza kuhusu inti yawâlawire, nanga wapata nafasi kuludira noko. ¹⁶ Fala kwasa javyo, ewo wakiwa nawo hamu kufika inti ngema pakulu, inti ya mbinguni. Ndimana Mwenyezimungu aawona haya kwitiwa Nlungu wawo ewo. Kusema kweli, iye kawatengezera kaya yawo.

¹⁷ Julu ya kwamini, Iburahima paayereriwe, ákiwa tayari kunlavya mwanawe Izaki awe kafara. Ire waâpewe tamaa, kanleva kuwa kafara mwanawe mmoja noyo tu basi, ¹⁸ ingawa kâmbiriwa mida kuwa: “Julu ya Izaki ndi kauja kulawirira ujukulu wako.” ¹⁹ Iburahima kamini kuwa Mwenyezimungu ákiwa na uwezo wakanludisira uhai anta afwe. Na ka ukweli, kinyume, ilanda kampokerera afwire futi.

²⁰ Julu ya kwamini, Izaki kâwajanliya kuhusu mambo akija kuwakuna mbere wanawe Yankubu na Ezau.

²¹ Julu ya kwamini, Yankubu, suku aba kábula yakufwa, kâwajanliya wana wa Yusufu mmoja-mmoja. Neye akimwabudu Mwenyezimungu kuno enyamire nkongojo wake.

²² Julu ya kwamini, Yusufu paawere karibu kufwa, kâkumbukira tamaa yakuwa ujukulu wake ukuja kulawa Miswiri uludira kwawo. Ndimana kâwalaizira wanawe vyawakijuzi kutenda makongolo ake.*

²³ Julu ya kwamini, wawaze Musa, bandi yakumpongola mwana wawo, wanfisa kwa muda wa myezi mitatu. Wámmona toto ire kuwa mwema pakulu na kwa sababu ya kwamini kwawo, awopire shuruti ya nfalume.

²⁴ Julu ya kwamini, Musa paakurire, kâkatala kutukuziwa kamba munu bora pakulu kwa sababu ya kuwa njukuluwe Firyauna nfalume wa Miswiri. ²⁵ Kwake iye kawona kuwa vyema pakulu kutabika na wanu wa Mwenyezimungu koliko kufurahira mambo a dambi kwa muda aba. ²⁶ Iye akiwaza kuwa kutabika kwa kufezeyiwa kamba vyaaja kutabika Almasihi, ndi bora pakulu koliko mali piya a Miswiri. Akiwaza javyo konta akirindira kupata tuzo mbere.

²⁷ Julu ya kwamini, Musa paalawire Miswiri opire kukimiwa ka nfalume. Kahitamili kamba ari kummona Ire sawoneka†.

²⁸ Julu ya kwamini, Musa kâwambira walziraeli wasasanyire damu mmiryango mwawo ipate Mwenyezimungu, paasaka kuntuma Nzulairi

* **11:22** Kâwambira kuwa suku moja walziraeli wakúja kuludira kwawo, ndimana wajuzi wasamise makongolo ake. † **11:27** “Ire sawoneka” ndi Mwenyezimungu.

kuwolaya wana watanzi wa WaMiswiri, asiwolaye wana watanzi wa walZiraeli.

²⁹ Julu ya kwamini, walZiraeli wâloka Bahari Nyeundu, wapita kati-kati ya bahari pakukama maji. Fala waMiswiri, pawakenekeze kutenda novire, wazama, wafwa piya.

³⁰ Julu ya kwamini, ukuta wa Yeriko bandi ya kuzunguriziwa muda wa suku saba, ûgwa.

³¹ Julu ya kwamini, reba wakwitiwa Rahabu kâwapa mamburo manasonde wa Iziraeli, ndimana aafwire pamoja na ware sawakinsikiriza Mwenyezimungu.

³² Mwaja, musaka nukwambireni kinani tena? Wakati uniwera aba, nanga nukwambirani kuhusu Gidiyoni, Baraki, Samsoni, Yefta, Daudi, Samuweli, pamoja na minabii wengine. ³³ Ewo, kwa kuwa wâmwamini Mwenyezimungu, wâwashinda mafalume wengine, wâtimiza sharia ya Mwenyezimungu, na wâpata Mwenyezimungu vyaawapere tamaa. Awawasire masimba kuwaduru, ³⁴ wâzimisa moto mwingi wawenye, wakinusurika mmakono mwa ware wakisaka kuwolaya na mapanga. Ingawa wâveya, wâlawirira kuwa na nguvu, wâlawirira kuwa masurudadu wakofya mpaka wâwashinda masurudadu wa inti nyengine. ³⁵ Wanawaka wakifwiriwa fala kwa kumwamini Mwenyezimungu wâwapokerera wafwi wawo, wafwi-wo waludira uhai.

Wanu wengine, kwa kunfulata Mwenyezimungu, wâkatala kufunguriwa nkalaboshu, ndimana wêbiwa mpaka kufwa. Watenda javyo ipate waludisiriwe uhai wapate mainsha meema pakulu. ³⁶ Wengine wâtabika na matusi na kukonyoriwa, wengine wâfungiwa na alucema na wâtaiwa nkalaboshu. ³⁷ Wengine wâkipanjiwa na mawe mpaka kufwa, wengine wâkibaluriwa kati-kati, wengine wâkulaiwa na upanga. Wengine wâkenenda wakisamasama, wakivalanga masambala a kondoo au a mbuzi, newo wâkiwa wakosofu pakulu, wakitabishiwa na wakopepesiwa. ³⁸ Wanu-wo ulumwengu-wu auwajuzire. Wâkipayapaya nlanga na mmyango, wakiinshi mmajonga na mmaondo kamba wanu wakutira.

³⁹ Wanu ware piya, ingawa wâjibisa ka Mwenyezimungu kwa kwamini kwawo, fala novyo-sivyo, awapokerere vyawapewe tamaa. ⁴⁰ Evi vikuna kanta Mwenyezimungu katipangira kinu cema, kuwa bila ofwe, wasikamilike.

12

Mwenyezimungu ndi Baba wetu

¹ Sambi, kwa kuwa tizunguriziwa na kundi ra mashahidi, tukeni tase piya vitendo vitikataza vyatijuzi kutenda, tase dambi iri kutizwiriza pakulu. Tukeni tituwirire kwa kuhitamili njira ituriwe mbere yetu ofwe. ² Tukeni tizidi kunnang'aniza Insa, kulongoza kwamini kwetu, tangu mwanzo mpaka mwinsho. Iye kahitamili kutabika pansalaba, aimmwerire aibu, kwa sababu ya radi ituriwe mbere yake. Epa sambi kecala mahala bora upande wa nkonu nririo wa kiti ka Mwenyezimungu.

³ Aye, tunzani sana-sana kuhusu iye, kawavumírira pakulu wamadambi wakintendera husuma, ipate musisokere, wala isukulaweni niya. ⁴ Kamana vita yenu yakubishana na dambi, amunamba kufika wakati wa kuvumirira

mpaka wanu wakuulayeni. ⁵ Kwasa javyo, amukumbukira usowezi urimbisa moyo? Muriwala caakwambireni Mwenyezimungu konta umwe muwa wanawe? Mandiko Matakatifu* akwamba:

“Mwanangu, fikiri sana-sana Mola paakolotera makosa ako. Iye paakusutumumu, usiuzunike.

⁶ Konta Mola awolotera makosa ware waawapenda. Piya waawapokerera kuwa wanawe, iye ndi wawasutumumu†.”

⁷ Ndimana Mwenyezimungu paakusutumuni, vumirirani. Mwenyezimungu akuwonani kamba wanawe. Na kweli, mwanani sasutumumiwa na wawaye? ⁸ Wasimana piya wásutumumiwa. Ndimana, ikiwa aakusutumireni, ilanda kamba mwana wakuningana, ailanda kamba muwa wanawe wakweli. ⁹ Visitoshe, wawa zetu mulumwengu-mu watisutumumu na atasa kuwasifu. Futi ofwe atinsikiriza Baba wetu wa mbinguni tipate kuinshi vyema? ¹⁰ Wawa zetu mulumwengu-mu watisutumumu kwa wakati aba, kwa ngano zawo zawawona kuwa ngema. Fala Mwenyezimungu atisutumumu kwa vyema vyetu wanyewe, ipate tiwe watakatifu tinlande iye. ¹¹ Basi, mulumwengu-mu kila mara patisutumumiwa ponse, tíwona kuwa kitendo cakutipa uzuni, acitifuraisha mmyoyo mwetu. Fala wapatire kusilimuka kwa kusutumumiwa na Mwenyezimungu, mwinsho wápata thawabu ya kuinshi kwa ukamilifu na usalama.

¹² Kwa javyo, lamukani muririmbise murolore muwe na nguvu. Rimbisani malundi enu mepepe-wo, musiteteme! ¹³ Enendani njira yakoloka ipate musizidi kuremala, ila mupone.

Musiture minyongo rehema ya Mwenyezimungu

¹⁴ Sakulani namuna za kuinshi kwa usalama na wanu piya na nshugulikireni Mola, konta saanatenda javyo, aakidiri kummona. ¹⁵ Rikengereni musiture minyongo rehema ya Mwenyezimungu. Rikengereni, nkati yenu asilawirire munu wakuwa na sumu kamba utupa, kuwatenza wenziwe wengi kwingira haramu. ¹⁶ Rikengereni nkati yenu asilawirire munu sharati, au kamba vyawere Ezau, saana inshima na vinu takatifu. Iye, kwa kupata finga moja tu basi ya cakurya, kápereka haki yake ya utanzi kupongoriwa. ¹⁷ Mukwijiwa kuwa mwinsho kadāi haki yajanliiwe na wawaye, fala kákataririwa. Aakidirire kupindula vyaâtendire, ingawa kasakula haki yake kuno akinlawa masozi mengi.

¹⁸ Umwe ámuri kamba walZiraeli wáfikire karibu ya Mwango wa Sinayi ukilawa malulimi a moto. Newo úfinikiwa kupi na giza, kuno mepo ikivunga thi-thi, ¹⁹ baramanda ikivuma, na shauti ya Mwenyezimungu íkisowera mpaka wakintafadali wakamba: “He! Atikidiri kusikira tena usowezi wake!” ²⁰ Ewo awákidirire kuhitamili ámuri ya Mwenyezimungu ikisema javi‡: “Munu au ndudu asaka kukumbula mwango ure onse apanjiwe na mawe mpaka afwe.” ²¹ Víkunire kuMwango wa Sinayi, anta Musa noyo vímopepesa, akamba§: “Nankutetema, wofi!”

* **12:5** Ona Ayuba 5:17; Usowezi 3:11. † **12:6** Ona Usowezi 3:12. ‡ **12:20** Ona Kulawa 19:12-13.

§ **12:21** Ona Kumbukumbu 9:19.

²² Fala umwe mufika karibu ya Mwango wa Ziyoni na Yerusalemu ya binguni, kaya ulu yekala Mwenyezimungu hai, mahala kawari malaika laki-ka-malaki. ²³ Mufika kujamati ya wana wakwanza kupongoriwa*, mazina awo andikiwe mbuku paandikiwe mazina a ware wóka mbinguni. Mufika karibu ya Mwenyezimungu, mwenyé kuwalamula wanu piya. Mufika novyo karibu ya róho za wanu wa shariya walawirire sambu kuwa makamilifu. ²⁴ Epa, mufika karibu ya Insa, mwenyé kupatanisa kwa miyadi mipya. Mufika karibu ya damu yake itawanyike, iri na uwezo pakulu zaida ya damu ya Abeli.

²⁵ More-more, musikatare kunsikiriza ári kusowera! Kamana, ikiwa ware wakatare kunsikiriza Musa apereke habari za Mwenyezimungu, awanusurike kuhukumiwa, futi ofwe! Tikuja kuhukumiwa pakulu, tikitula minyongo Mwenyezimungu asowéra nofwe binguni! ²⁶ Wakati wa Musa, shauti ya Mwenyezimungu itetemesa ardhi, fala sambu Mwenyezimungu katipa tamaa nkati ya Mandiko javi: “Nitetemesa inti tena, wala si inti basi, na bingu neyo novyo.”

²⁷ Sambu, usemi wa “tena” utolotera kuwa vinu vyumbiwe vyonse vitetemisiwa na vilainika, ila vibaki ndi vire savitishiwa. ²⁸ Basi, kwa kuwa tipokerera ufalume sautishiwa, tishukuru. Kwa javyo, tintumike Mwenyezimungu kwa namuna zakumwajibu iye, kwa kumwinshimu na kumopa. ²⁹ Kamana Nlungu wetu kawa kamba moto nkali vyaupoteza.

13

Namuna za kumwajibu Mwenyezimungu

¹ Kamba munu na nduye, zidini kupendana. ² Musase kuwakaribisha wayeni, kontu kwa kutenda javyo, wamojawapo wafikirira kuwapokerera malaika mmanyumba mwawo bila kwijiwa. ³ Watendereni huruma wanu wafungiwe na muwasaidiye, onani kamba mufungiwe nawo pamoja. Watendereni huruma wanu wari kutabika, tulani kamba utabika mwiri wenu pamoja newo. ⁴ Wanu piya wajuzi wainshimu ndowa. Kusema kweli, muka na nlume wenarirane, kamana Mwenyezimungu akúja kuwahukumu waz-inzi pamoja na masharati. ⁵ Vinu vyakuuziwa na nzuruku, zidini kutowa kuperereza. Vikutosheni vinu vyamuri nawo, kamana Mwenyezimungu kasema: “Sukwasa futi, wala sukutipuka.” ⁶ Ndimana na hakika tikwamba javi*:

“Mola ndi anisaídiya, omi sopa kinu.
Mwanadamu anitenda kinani cakunyata?”

⁷ Wakumbukireni wakulungwa wenu wákwerezeni habari za Mwenyezimungu. Tunzani vyawainshire na vyawafwire. Wafulatizeni kwamini kwawo. ⁸ Insa Almasihi ndi mmoja noyo, ijana na rero na milele-yi. ⁹ Musiwasikirize wanu wafúnda inlimu nyengine jisijisi wakupotezani njira ya ukweli. Cisáka kukupani nguvu mmyoyo myenu siyo shuruti kuhusu camujuzi kurya. Kwa kifulata nozo shuruti-zo, tangu hapana munu apatire faida yake. Ila cisaka kukupani nguvu ndi rehema za Mwenyezimungu. ¹⁰ Walongozi wa dini wákutumikanga muEma Takatifu ya Mayahudi awana

* **12:23** “Wana wakwanza kupongoriwa” ndi wenye kwamini. * **13:6** Ona Zaburi 56:4, 11; Zaburi 118:6.

haki ya kurya vilaviwa kafara yakutukuza† mahala petu pakwambudu. ¹¹ Nkulungwa wa dini mara moja kila mwaka‡ ákisukulanga damu ya manyama, akipereka ka Mwenyezimungu Mahala Patakatifu Pakulu, iwe kafara ya kufuta madambi. Fala mwiri wa nozo nyama-zo úkociwanga panja ya kaya ulu ire. ¹² Ndimana Insa, kwa ajili ya kuwaswafi wanu madambi julu ya damu yake, neye novyo kâfwa panja ya kaya ulu. ¹³ Basi, tukeni tikawe pamoja naye panja ya kaya ulu-yi§, tiwe tayari kukejeliwa kamba vyaakejeliwe iye. ¹⁴ Kamana mulumwengu-mu, atina kaya ya milele, fala tírindira kaya yatija kuwa nawo mbere. ¹⁵ Basi, julu ya Insa, daima tilavye kafara ka Mwenyezimungu kwa kuntukuza, kwa kwakikisha zina rake na kanywa zetu. ¹⁶ Fala musiriware kutenda meema na kumera, kamana ezo ndi kafara zakumwajibu Mwenyezimungu.

¹⁷ Wasikirizeni wakulungwa wenu kwa kufulata ámuri zawo, kamana ewo washugulikira daima faida zenu, wakijiwa kuwa wajuzi kujibu ka Mwenyezimungu. Waseni watende kazi kwa radi. Musiwatenze kwisa moyo, konta javyo aiwepo faida kwenu umwe.

¹⁸ Musase kutilebelela duwa. Tanawo uhakika kuwa myoyo yetu iwa swafi, konta tísakula kutenda meema kwa kila hali. ¹⁹ Visitoshe, nukulebelani ka moyo wangu piya, munilebelele duwa ipate Mwenyezimungu aniludise niwe pamoja namwe kwa suku karibu.

Duwa ya mwinsho

²⁰ Sambu, Mwenyezimungu mwenyé usalama, anfuture ka wafwi Mwenye wetu Insa, Nsunga nkulu wa makondoo, julu ya damu yakikisha miyadi ya milele, ²¹ nínlebelu akupeni piya vinu vyema-vyema mutimize nafsi yake, muktenda vyavimwajibu iye, julu ya Insa Almasihi. Iye atukuziwe daima milele! Aamina.

Masemo a mwinsho

²² Wanduzangu, nukutafadalini mupokerere ewu usowezi-wu kwa radi kamana nukwandikirani kwa usemi aba. ²³ Mukwijiwa kuwa nduyetu Timotiyu kafunguriwa nkalaboshu. Iye, akija saninamba kulawa kuja kukuwonani, tikuja onse. ²⁴ Salamu zawo wakulungwa wenu piya pamoja na watakatifu piya. Wanduzetu wa Italiya wakuperekerani salamu.

²⁵ Rehema iwe pamoja namwe piya.

† **13:10** Ona aya 15. ‡ **13:11** Usemi wa “mara moja kila mwaka” aupo nkigeregu ila ikweleweka javyo. § **13:13** Mana ake ndi kulawa mahala patikiwa bila tafauti.

Waraka ya Yakubu

Mwanzo

Eyi waraka-yi ifunda namuna vyawajuzi kuinshi wenye kwamini. Ikwereza novyo kuhitamili, kwamini ka ukweli, na faida ya kutunza lulimi na namuna ya kutumira imani kuripereka kutenda nafsi ya Mwenyezimungu.

Eyi waraka-yi yandikiwa kiyasi ca mwanzo wa mwaka 40-50 bandi ya Almasihi. Andíke ndi nduye Insa, wakwitiwa Yakubu.

Salamu

